# Nipashe

Jumanne Aprili 6, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580542

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Wadau** wapongeza uteuzi, lakini jinsia izingatiwe

UKURASA 2



**Vyama** saba vyakosa sifa uchaguzi mdogo Muhambwe

UKURASA 4

**De Gea sasa rasmi kuondoka Man United**

UKURASA 21



# Vigogo CHADEMA wamfagilia Samia

• **Mbowe** amkumbushia suala la katiba mpya... *Endelea uk.2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 3**

**WAGOMA VIFAA TIBA KUHAMISHWA KWENYE KITUO CHAO**

KUNDI la wananchi wa kijiji cha Nagaga, Kata ya Nagaga, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi...

**UKURASA WA 4**

**JINSI MKURUGENZI WA TPDC ALIVYOPONEA TUNDU LA SINDANO**

NI kama kuponea kwenye tundu la sindano au bahati ya mtende kwa Mkurugenzi wa Shirika la...


## Mufti ateua vigogo nafasi nyeti

UKURASA 5



Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Mbezi Beach, Dar es Salaam, Allen Mbiso, akibatiza mmoja wa watoto jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**



## Milima, mabonde safari ya Kamishna Mkuu TRA

UKURASA 3


**MICHEZO** **SIMBA SC YATISHA VIGOGO CAF** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Watoto wakibembea kusherehekea Sikukuu ya Pasaka katika Ukumbi wa Yangeyange Kitunda, Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wadau wapongeza uteuzi, lakini jinsia izingatiwe

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU mbalimbali wamempongeza Rais Samia Suhuhu Hassan kwa uteuzi wa makatibu wakuu, manaibu katibu wakuu na wakuu wa taasisi mbalimbali za serikali huku wakimuomba kuzingatia jinsia kwenye uteuzi wake.

Katika uteuzi wa juzi usiku, kati ya wateule 49 wanawake ni tisa huku nafasi za wakuu wa taasisi za umma hakuna mwanamke hata mmoja.

Walisema pamoja na walioteuliwa kuwa na sifa za kitaaluma, lakini bado jicho linatakiwa litupiwe pia katika kundi la wanawake wenye uwezo wa kushika nyadhifa hizo.

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema wanawake ni miongoni mwa makundi ya watu wenye uwezo na watafanya vizuri zaidi endapo wataaminiwa na kushika nafasi mbalimbali za umma.

"Mara nyingi nafasi za makatibu wakuu, wakuu wa taasisi za serikali lazima wawe na 'background' (historia) ya utumishi wa umma na sio wanasiasa na ndicho ambacho tunakiona kwa Rais Samia akikizingatia," alisema na kuongeza:

"Wengi tunaowaona wanatoka humo humo na ni sura zile zile, isipokuwa bado tunaona kwamba sura za wanawake hazipo."

"Tunafahamu kwamba kwa kuwa Rais Samia alikuwa katika serikali iliyopita, viongozi wengi anawafahamu na ndio maana labda anarudisha walewale isipokuwa kwa kuwapangua kila mmoja kukaa katika taaluma yake sahihi," alisema.

"Bado tunaona umuhimu atupie jicho lake pia kwa wanawake na huu ndio mjadala mkubwa unaoendelea mitandaoni, wapo wengi huko kwenye taasisi za umma na wana uwezo awaangalie na wao."

Kadhalika Shaibu alisema: "Tangu enzi za TANU kumekuwa na shida ya kutotambua wanawake kwenye taasisi kubwa japo wako wengi tu huko ndani ya umma na wana uwezo mkubwa, japokuwa tunaamini bado ni mapema, lakini na wao waangaliwe."

Hata hivyo, alimpongeza Rais Samia kuchukua hatua ya haraka kurekebisha nafasi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC).

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Rose Reuben, alisema, kuna haja ya kuzingatia makundi yote katika uteuzi wa nafasi mbalimbali.

"Walioteuliwa ni walewale japokuwa wamebadilishwa badilishwa, lakini bado tunaona wengi wao ni wanaume. Mimi nafikiri katika nafasi kama hizi kuna haja ya kuzingatia makundi yote, wanaume na wanawake, vijana, wazee na hata wenye ulemavu kwa sababu nao uwakilishi wao unahitajika," alisema Rose.

"Namini kwamba katika nafasi hizo wanazoteuliwa wanaume, hata makundi mengi wapo wenye uwezo mkubwa tu, kikubwa ni kutanua wigo badala ya kuangalia eneo moja tu. Ni matumaini kwamba kwa teuzi nyingine hili litazingatiwa."

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, alisema wanaamini hata wanawake wapata nafasi kwa sababu muda bado upo.

"Bado ni muda mfupi kusema wanawake wameachwa kwa sababu asilimia kubwa ya viongozi walioteuliwa ni wale waliokuwa katika nafasi zao, kinachofanyika ni kuwabadili kila mtu kukaa katika taaluma yake na wachache walirejeshwa ambao waliondolewa kutokana na uhitaji uliopo," alisema Dk. Kahangwa.

"Tunaona Rais anaunda serikali yake na kufanya marekebisho katika maeneo ambayo anaona pana shida na ndio maana tunaona baadhi wamerudishwa, jambo la msingi ni kila kiongozi kuwekwa kwa kuzingatia vigezo vya uzoefu na kwa taaluma husika."

Alimpongeza Rais Samia kwa kumrejesha Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, Dk. James Mataragio na kutengua uteuzi wa aliyekuwa ameteuliwa kushika nafasi hiyo Aprili 4, mwaka huu, Thobias Richard.

"Ninampongeza Rais Samia kwa kuchukua uamuzi wa haraka kufanya mabadiliko TPDC, tunaomba hata wale wanaofanya 'vetting' (chagua) wasimpotoshe kiongozi wetu," alisema Dk. Kahangwa.

Jumla ya makatibu wakuu, manaibu katibu wakuu na wakuu wa taasisi walioteuliwa Aprili 4, mwaka huu kushika nafasi hiyo ni 49 na kati ya hao wanawake wakiwa tisa.

Katika uteuzi huo, makatibu wakuu wakiume ni 20, wa kike ni wanne.

Manaibu katibu wakuu wa kiume ni 20 na wa kike ni watano, huku wakuu wa taasisi wakiwa tisa wote wa kiume.

Kwa upande wa mawaziri, wanawake mpaka sasa wako watano kati ya 24, na manaibu waziri pia ni watano.

# Vigogo CHADEMA wamfagilia Rais Samia

**Na Mwandishi wetu**

VIONGOZI mbalimbali wa kisiasa kususani wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ameanza vizuri katika kutekeleza majukumu yake.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Feeman Mbowe, amemshukuru na kumkumbusha Rais Samia kuhusiana na kuendeleza mchakato wa kuipatia Tanzania katiba mpya.

Katika ukurasa wa tweeter wa Rais, Samia alituma ujumbe wa Pasaka wa Watanzania "Nawatakia Watanzania wote Pasaka njema, tudumishe ufufuko wa Yesu Kristo huku tukiliombea taifa letu la Tanzania kudumisha amani, upendo na mshikamano.Tuendeleze jitihada za kuijenga nchi yetu kwa kuchapa kazi kwa juhudi na maarifa."

Miongoni mwa viongozi walioandika ni Mbowe "Mama Samia nimejitahidi kubana hisia zangu kwa muda, nimeshawishika kukushukuru kwa kututakia kheri ya Pasaka sisi Wakristo. Jamii ya CHADEMA tunashukuru ila napenda kutoa ombi la Pasaka tupatie katiba mpya."

Naye, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Arusha, Godbless Lema aliandika " Ukisoma comments (maoni) hapa, utaona kuwa watu wana matumani na wewe. Watu hawahitaji vitu bila uhuru, haki, usawa na upendo. Kila mara unapotafakari maendeleo usiache kuamini kuwa maendeleo ya kwanza ya binadamu ni haki. Kauli zako zina matumani. Leadership is love (uongozi ni upendo).Heri ya Pasaka."

Naye, aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Dar es Salaam, Henry Kileo, aliandika " Tulikuwa tuna msongo wa mawazo, akili zikadumaa, kwa kifupi tulichakaa tukawa hoi bin taabani ghafla tumeanza kuwa na nuru za stress (msongo wa mawazo) zinapotea kila uchwao."

Naye, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana wa Chadema (BAVICHA), Julius Mwita, " Amina Mh Rais, nasi tunakuombea ili usitusahaulishe sana suala la Katiba Mpya, na ufutwaji wa kesi za kubambikiwa wananchi wako. Nchi hii inayofuata mfumo wa vyama vingi, nikuombe kwa mujibu wa sheria uruhusu sasa vyama vifanye siasa kwa uhuru bila kubugudhiwa."

Kwa upande wake, aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Absalom Kibanda, aliandika " Rais mpya, Mwanzo Mpya. Tuna jambo letu mama, uwe na Pasaka njema Mh. Rais. Sasa tunatembea kwa kujiamini na tukiwa huru kiakili na kifikra."

Naye, Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye aliandika " Upendo huunganisha taifa.Asante kwa upendo wako kwa watu wako. Mapumziko mema ya Pasaka."

Naye, Profesa Willy Makundi aliandika "Heri ya Pasaka Rais wetu mama Samia Suluhu, Bwana Yesu aliyefufuka siku kama leo akubariki na familia yako uendelee kutupa matumaini ya uhuru, haki na afya haswa dhidi ya corona. Baada ya muda mrefu nimeamka Pasaka hii na matumaini kwa nchi yangu."

# Wananchi wagoma vifaa tiba kuhamishwa kwenye kituo chao

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

KUNDI la wananchi wa Kijiji cha Nagaga, Kata ya Nagaga, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi, mkoani Mtwara, limevamia kituo cha afya cha kata hiyo na kuzuia uhamishwaji wa vifaa tiba kwenye kituo hicho kwenda kwenye hospitali ya wilaya.

Wananchi hao walizuia vifaa hivyo kuhamishwa ikiwamo kiti cha kung'olea meno pamoja na mashine ya kufulia hali iliyosababisha tafrani kwa zaidi ya saa moja kati ya wananchi hao na timu ya idara ya afya iliyofika kituoni hapo kuhamisha vifaa hivyo.

Hatua hiyo imekuja baada ya timu maalumu ya afya ya halmashauri hiyo kwenda katika kituo hicho kuhamisha vifaa hivyo ikidai kupewa agizo na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Changwa Mkwazu, kuhamisha na kwenda kuvifunga katika hospitali ya wilaya iliyopo kijiji cha Mbuyuni.

Tukio hilo limetokea jana na wakazi hao walizungumza na gazeti hili na kueleza kuwa wameamua kuzuia vifaa hivyo kwa kuwa hawakubaliani na uamuzi huo uliofanywa na halmashauri yao kwa sababu bado wananchi wanavihitaji kwa ajili ya kuwahudumia.

Mkazi wa kijiji hicho, Zuhura Masudi, alisema kama vifaa hivyo vilitolewa msaada katika kituo hicho cha afya vitaendelea kuwapo hapo na kutoa huduma kwa ajili ya wananchi wa kata hiyo na sio vinginevyo.

Naye Mzuluni Hassani, alisema suala la vifaa hivyo kushindwa kufungwa katika kituo hicho cha afya kwa muda mrefu, wananchi walishaanza kujega jengo maalumu la kuvifunga kwa nguvu zao wenyewe.

Alisema walishafyatua tofali na kusomba mchanga kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo maalumu la kufunga vifaa hivyo.

Mwenyekiti wa kamati ya afya ya kata, Hassani Mkata, alisema kamati haijapewa taarifa yoyote na uongozi wa halmashauri kuhamishwa vifaa hivyo.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Halmashauri ya wilaya ya Masasi, Dk. Miriam Cheche, alisema vifaa tiba hivyo vilitolewa msaada miaka minne iliyopita katika kituo hicho, lakini havikuweza kufungwa.

Alisema wiki hii walipewa agizo na Mkurugenzi wa halmashauri kwenda katika kituo hicho na kuondoa baadhi ya vifaa hivyo kwa kile kilichoelezwa kuwa vimekaa hapo kwa muda mrefu bila ya matumizi.

"Sisi tumekuja hapa leo kwa ajili ya kuhamisha vifaa hivi, lakini kwa sababu wananchi wametugomea kuvichukua tutarudi kwa mkurugenzi kumweleza jambo hili," alisema Dk. Cheche.

Alisema kuwa vifaa hivyo vilishindwa kufungwa katika kituo hicho cha afya kutokana na kukosekana kwa jengo maalumu la kuvifunga.

# Milima, mabonde safari ya Kamishna TRA

**Na Salome Kitomari**




SAFARI yenye milima na mabonde ya utumishi wa umma ya Alphayo Kidata (pichani), imemfikisha kwenye nafasi aliyoanzia kazi yake mwaka 2016.

Kidata katika Serikali ya Awamu ya Tano alianza na nafasi ya Kamishna wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), ambayo alidumu kwa muda mfupi na baada ya kuhama sehemu tofauti, amerudishwa tena katika nafasi hiyo.

Ndani ya miaka sita Kidato alipitia misukusuko ya utumishi wa umma kwa kuhamishwa vituo vingi vya kazi hadi kuvuliwa hadhi ya ubalozi na kurudi kutumikia ngazi ya mkoa.

Mwaka 2015 alikuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, na baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani aliteuliwa kuwa Kamishna wa TRA nafasi aliyodumu nayo hadi Machi 2017.

Machi 25, mwaka 2017, Hayati Rais John Magufuli, alimteua Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Charles Kichere, kuwa Kamishna Mkuu wa TRA akichukua nafasi ya Kidata.

Aidha, Kidata aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ikulu nafasi aliyodumu hadi Januari 11, mwaka 2018, alivyoteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Canada na kudumu kwa miezi 11.

Novemba 8, mwaka 2018, Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Faraji Mnyepe, alitoa taarifa kwa umma kuwa Rais Magufuli ametengua uteuzi na kumrejesha nchini aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Canada, uamuzi ulioanza Novemba 5, mwaka huo.

Alisema pia Kidata ameondolewa hadhi ya ubalozi.

Septemba 20, mwaka 2019, Kidata aliteuliwa kuwa Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, akichukua nafasi ya Dk. Jilly Maleko, aliyeteuliwa kuwa balozi.

Juzi Kidata alirejeshwa tena kwenye nafasi yake aliyoitumikia mwaka 2016, na ni miongoni mwa watumishi wachache wenye historia ya kuelezea safari yao ya utumishi wa umma, kwa kupita sehemu nyingi za kiutumishi ndani na nje ya nchi.


Tumehama!

Tunapenda kuchukua fursa hii kuwajulisha wadau wetu wote na jamii kwa ujumla kwamba ofisi zetu zimehamia kwenye jengo jipya.

equinor

**Kwa sasa tunapatikana kwenye eneo lifuatalo;**
Namba 429, Mtaa wa Mahando
Jengo A
Msasani Peninsula
Dar Es Salaam
Tanzania

Simu; + +255 684 226203 / + 255 764 958550




Shaping the future of energy

www.equinor.com

## Ndaki acharuka mnada kukosa mapato miaka 4

**Na Halima Ikunji,** IGUNGA

WAZIRI wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amewasimamisha kazi msimamizi wa mnada wa Igunga mkoani Tabora, Juma Athumani, kwa tuhuma za ubadhilifu wa fedha na ametoa maelekezo kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga kuondolewa Ofisa Afya ya Mifugo, Mohamed Kifamba.

Pia, amemtaka Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Igunga, kuwaondoa askari polisi waliokuwa wakisimamia mnada huo kutokana na tuhuma za ubadhirifu.

Ndaki alichukua hatua hiyo jana wakati wa ziara yake katika mnada huo baada ya kubaini kutokuwapo nyaraka za kumbumbuku za tozo na mauzo ya mifugo walioingia na kutoka katika mnada huo kwa muda wa zaidi ya miaka minne.

Waziri huyo alisema kwamba kukosekana kwa kumbukumbu hizo kumeishababishia serikali hasara ya fedha nyingi jambo ambalo haliwezi kuvumilika. Alisema licha ya kuwasimamisha kazi watuhumiwa hao alivitaka vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma za ubadhirifu wa mapato ya serikali yaliyopotea kwa kipindi cha miaka minne.

"Nasema haiwezekani, haiwezekani serikali haiwezi kuvumilia kuendelea kukosa mapato wakati kila siku ya minada inapofanyika na watu wachache wakiiba," alisema Waziri Ndaki.

Amemwagiza Katibu Mkuu wizara yake, kupeleka watu wa ukanguzi na kufanya uchunguzi wa kina kwa ajili ya kuangalia mapato ya serikali yaliyopotea katika kipindi hicho.

Pia, alimsimamisha kazi msimamizi wa mnada huo, Haidari Mwinyihija, kuendelea kuuangalia mnada huo wakati serikali ikiendelea na utaratibu wa kumpata mtu mwingine wa kufanya kazi hiyo.

Waziri Ndaki alimtaka Mkurungezi mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, kupeleka ofisa mifugo mwingine na mkuu wa polisi wa wilaya hiyo kupeleka askari wengine katika mnada huo.

# Vyama 7 vyakosa sifa ubunge Muhambwe

**Na Deogratius Nsokolo,** KIBONGO

Vyama saba vya siasa kati ya kumi vilivyochukua fomu kugombea ubunge katika Jimbo la Muhamwe wilayani Kibondo Mkoa wa Kigoma, vimeshindwa kukidhi vigezo vya kugombea ubunge katika katika uchaguzi mdogo wa ubunge unaotarajiwa takaofanyika Mei 2, mwaka huu.

Vyama ambavyo vimekidhi vigezo na wagombea wake kuteuliwa ni Julius Masabo wa ACT-Wazalendo, Dk. Florence Samizi wa CCM na Philipo Fumbo wa Democratic Party (DP).

Msimamizi wa uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe, Diocles Lutema, alivitaja vyama ambavyo vimeenguliwa baada ya kushindwa kukidhi matakwa ya kisheria kuwa ni UPDP, CCK, Demokrasia Makini, ADC, SAU, AAFP na CHAUMA.

Alisema CHAUMA kupitia kwa mgombea wake, Bernard Ngarama hakikurejesha fomu, huku vyama vingine vikikosa sifa za kugombea kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutokuwa na picha, kukosea kujaza fomu na kutopata wadhamini.

Hata hivyo, mgombea wa chama cha ADC, Shaban Itubu, alisema atakata rufni kupinga uamuzi huo kwa kuwa anaamini amekidhi vigezo vyote vilivyohitajika.

Naye Mohammed Juma ambaye aliomba kugombea kupitia tiketi ya Demokrasia Makini, alisema ameenguliwa kwa madai ya baadhi ya wadhamini walioorodheshwa kwenye fomu yake hawapo kwenye daftari la mpigakura, na kwamba atakata rufaani kupinga uamuzi huo.

Kwa upande wake mgombea kupitia CCM, Dk. Florence Samizi, alisema baada ya kupitishwa kuwa mgombea, kuwa anaamini atashinda katika uchaguzi huo kutokana na ubora wa ilqni ya chama chake ambayo ndio iliyochaguliwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

"Nawaomba wananchi wa Muhambwe mjitokeze kwa wingi katika mikutano ya kampeni, nashukuru nimeteuliwa, lakini tunahitaji ushirikiano wa kila mmoja ili kukirejesha kiti cha ubunge ndani ya CCM," alisema.

Naye Julius Masabo mgombea kwa tiketi ya ACT- Wazalendo, alisema hii ni fursa muhimu kwake na chama chake kuibuka washindi katika uchaguzi huo mdogo,na kwamba watafanya kampeni za kistaarabu na za kisasa zaidi kuhakikisha chama hicho kinashinda.

Uchaguzi katika Jimbo la Muhambwe unafanyika kufuatia kufariki kwa aliyekuwa mbunge wake, Hayati Atashasta Nditiye.



Naibu Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Pauline Gekul (kushoto) ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini Mkoani Manyara, akizungumza na Kamati ya Mfuko wa Jimbo ili kuchochea maendeleo ya kata nane za eneo hilo mwishoni mwa wiki.
**PICHA: GIFT THADEY**


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu Jumba Habraham Burasio anatangaza kupotea kwa kadi ya gari namba T371 AWN yenye majina ya Said Shehe Hamad.Taarifa imetolewa katika kituo cha Polisi Bukoba kwa jarada KAG/BUK/R-B/180124/2021.yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi.


# Jinsi Mkurugenzi TPDC alivyoponea tundu la sindano

**Na Salome Kitomari**

NI kama kuponea kwenye tundu la sindano au bahati ya mtende kwa Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC), Dk. James Mataragio, ambaye mara mbili amenusurika kung'olewa kwenye nafasi hiyo. Juzi usiku Rais Samia Saluhu Hassan, alimteua Thobias Richard, kushika nafasi hiyo na asubuhi ya jana alitengua uteuzi huo na kumrejesha Dk. Mataragio kuendelea nafasi hiyo.

Mkurugenzi huyo alishawahi kuondolewa kwenye nafasi hiyo na kupandishwa kuzimbani katika Mahakama ya Kisutu, lakini kwa amri ya rais alirejeshwa kwenye nafasi yake. Julai 22, mwaka 2019, Rais Hayati Dk. John Magufuli, alimwagiza Waziri wa Nishati kumrejesha kazini mara moja mkurugenzi huyo katika nafasi yake ya ukurugenzi ili aendelee na majukumu yake.

Dk. Mataragio alisimamishwa kazi na Bodi ya Wakurugenzi ya TPDC Agosti 20, mwaka 2016, kwa kile kilichoelezwa kuwa ni upungufu uliobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2015.

Machi 17, mwaka 2018, Dk. Mataragio alifikishwa mahakamani pamoja na vigogo wengine wanne wa TPDC kujibu mashtaka ya matumizi mabaya ya madaraka na kujipatia dola za Marekani 3,238,986.50 (Sh. bilioni 7.3).

Agosti 19, mwaka huu, aliachiwa huru na Mahakama ya Kisutu kutokana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), kutokuwa na nia ya kuendelea na mashtaka dhidi ya Dk. Mataragio na wenzake.

Dk. Mataragio na wenzake walidaiwa kati ya Aprili 8, 2015 na Juni 3, mwaka 2016, wakiwa watumishi wa umma kwa nafasi zao walitumia nafasi zao vibaya.

Ilidaiwa walibadilisha na kupitisha bajeti na mpango wa ununuzi wa mwaka 2014/2015 na 2015/2016 kwa kuingiza ununuzi wa kifaa cha utafiti cha Airborne Gravity Gradiometer Survey bila kupata kibali cha bodi ya wakurugenzi ya shirika hilo. Dk. Mataragio aliteuliwa Rais wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete kuwa Mkurugenzi wa TPDC, Desemba 15, 2014, akitokea nchini Marekani, akiwa Jiosayantisti Mwandamizi wa kampuni ya Bell Geospace, Huston, Marekani.

HABARI KITAIFA

# Mufti ateua viongozi nafasi nyeti

**Na Elizabeth Zaya**

MUFTI na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Sheikh Abubakar Zubeir, amefanya uteuzi wa Masheikh wa mikoa, makatibu wa mikoa wa Baraza Kuu la Waisalamu Tanzania (BAKWATA) pamoja na makatibu wa makadhi wa mikoa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwenye vyombo vya habari jana, Mufti amefanya uteuzi huo kwa mujibu wa Katiba ya Baraza hilo ya mwaka 1999 toleo la mwaka 2018.

**MASHEIKH MIKOA**

Masheikh walioteuliwa katika mikoa ya Arusha ni Shaban Juma, Kilimanjaro ni Mlewa Kimwanga, Dar es Salaam ni Alhad Mussa Salim, Dodoma ni Mustapha Rajabu, Lindi ni Mohamed Mushangani, Manyara ni Mohamed Kadidi, Mara ni Msabaha Ngabo na Geita ni Alhad Kabaju.

Masheikh katika Mkoa wa Mtwara ni Nurdin Mangochi, Singida ni Salum Mahami, Tanga ni Ali Luwuchu, Kagera ni Haruna Kichwabuta, Rukwa ni Rashidi Akilimali, Tabora ni Ibrahimu Mavumbi, Njombe ni Rajabu Msigwa , Simiyu ni Mahamoud Kalokola na Shinyanga ni Ismail Makusanya na Songwe ni Hussein Batuza

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Masheikh hao wanaungana na Sheikh Hassani Musa Kabeke wa Mwanza na Sheikh Mashaka Nassoro Kakulukulu wa Katavi ambao walishateuliwa awali.

Pia Baraza la Ulamaa limewakaimisha masheikh wapya kwenye mikoa ya Ruvuma, Ally Mahaba, Mbeya ni Msafiri Njalambaha na Iringa Said Al Abri.

Pia ilieleza kuwa, Sheikh Twaha Kilango wa Mkoa wa Morogoro na Sheikh Iddi Hassani Kiburwa wataendelea kukaimu nafasi zao mpaka pale Baraza la Ulamaa litakapofanya uteuzi rasmi kwa Mikoa hiyo.

**MAKATIBU WA BARAZA LA MASHEIKH**

Pia, Mufti amefanya uteuzi was Makatibu wa Baraza la Masheikh la Makatibu walioteuliwa ni kwenye mikoa ya Arusha Said Chudi, Kilimanjaro ni Taqdir Dhahabu, Dar es Salaam ni Ally Kizegero, Dodoma ni Buniamini Abdurabi, Njombe ni Saad Ally na Morogoro ni Ajali mlenga.

Mwanza ni Alhaji Masasi, Manyara ni Mwinyi Rashidi, Mara ni Salum Nyisuka, Geita ni Baharan Salum, Mtwara ni Abdulhafidh Kassim, Mbeya ni Abasi Mshauri, Singida ni Omary Ally na Tanga ni Juma Bakari.

Mikoa ya Kagera ni Najim Khalid, Kigoma ni Alhaji Sangi, Iringa ni Abdulrahim Ngole, Pwani ni Salmin Budap, Rukwa mbegu Hangolwa, Simiyu ni Hussein Mbaruku, Katavi ni Mussa Kazige, Tabora ni Jabu Said na Songwe ni Ally Mambea.

**MAKATIBU WA MAKADHI**

Masheikh walioteuliwa kwa Mkoa wa Arusha ni Mbaraka Mtonyi, Kilimanjaro ni Issa Juma, Dar es Salaam ni Abdulkarim Pazi, Dodoma ni Mohamed Sendoro, Morogoro ni Swalehe Lukanda na Mwanza ni Ramadhani Khamisi.

Mkoa wa Manyara ni Sheikh Adam Zubeir, Mara ni Kudra Migozi, Geita ni Hamisi Mlea, Mtwara ni Mussa Mwarabu, Mbeya ni Ally Furukutu, Singida ni Abdallah Takaza na Kagera ni Mikidadi Banobi

Wengine kutoka mikoa ya Kigoma ni Majaliwa Kagama, Iringa ni Abdalla Khalid, Rukwa ni Abdallah Katalango, Tabora ni Athumani Kabogota, Katavi ni Omari Kabwiri, Njombe ni Idd Gadau, Simiyu ni Kassim Mohamed , Songwe ni Hussein Juma, Tanga ni Ally Saleh.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mikoa mingine iliyobaki uteuzi wake utafanyika baadae.

# Bodaboda Dar wamkumbuka JPM

**Na Halfani Chusi**

MADEREVA wa pikipiki (bodaboda, wameonyesha kuumizwa na kitendo cha kuondokewa na Rais wao Hayati Dk. John Magufuli.

Wakizungumza katika maeneo tofauti tofauti ya jiji la Dar es Salaam, walisema katika kutetea wanyonge Rais Magufuli, hakuwaacha nyuma bodaboda kwa kile walichodai kupewa kipaumbele cha kufanyia kazi katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika kituo kipya cha mabasi Mbezi kilichopewa jina la Magufuli.

Walisema Rais Magufuli wakati anazindua kituo cha mabasi Mbezi, alihitaji kuona bodaboda wanapewa kipaumbele kupaki na kuchukua abiria maeneo hayo

Mmoja wa bodaboda, Jakobo Kilamba, alisema Rais Magufuli, aliwatujali na kuwatuthamin katika mambo mengi ikiwemo kuwaacha kuingia katikati ya Jiji.

"Uongozi wa Rais Magufuli, ndio uliofanya sisi bodaboda kuingia katikati ya Jiji na kuchukua abiria tofauti... awali tulikuwa tunazuwiliwa kuingia katika ya jiji, lakini kupitia uongozi wa mtetezi wa wanyonge Magufuri, tuliruhusiwa na mpka sasa tunaingia mjini bila tatizo."

Kwa upande wake, de4reva Suleiman, alisema amesikitshwa na kifo cha Magufuri na kumtaja kuwa ndie raisi pekee aliyejenga barabara kwa kiwango ambacho kilifanya bodaboda kufanya kazi kwa furaha kutokana na uzuri wa miundombinu.

"Kinachifanya nimkumbuke ni kitendo cha kuboresha barabara za mtaa pamoja na kujenga barabara mpya ambazo sisi ambao tunatoa huduma za usafirishaji imetuwekea urahisi mkubwa sana sambamba na kutuepushia kuharibika kwa vyombo vyetu kwa kisingizio cha ubovu wa barabara"

Kwa upande wake Haji Saluum, alisema anamkumbuka kwa kuweka jituhada katika kupunguza vitendo vya wizi wa pikipiki katika utawale wake sambamba na kuimarisha ulinzi na usalama tofauti na awali.


PONGEZI



Mhe. Balozi Hussein A. Kattanga
Katibu Mkuu kiongolzi

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa **Benki ya TPB** wanaungana na Watanzania wote kumpongeza **Mhe. Balozi Hussein A. Kattanga** kwa kuapishwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

*Hongera sana.*

TpbBank Grow with us
www.tpbbank.co.tz info@tpbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ripoti ya CAG itumike kuimarisha uwajibikaji

**KUNA** hatua kadhaa ameanza nazo Rais Samia Suluhu Hassan kuhakikisha uwajibikaji unatawala miongoni mwa watendaji wa serikali anayoiongoza baada ya kurithi mikoba ya mtangulizi wake, Hayati Dk. John Magufuli.

Hatua hizo ni pamoja na kumsimamisha kazi Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari (TPA) ili kupisha uchunguzi kutokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20 kubaini upotevu wa mabilioni ya shilingi katika mamlaka hiyo.

Baada ya kupokea ripoti hiyo nyeti Machi 28 mwaka huu, Rais Samia pia aliagiza kufanyike ukaguzi maalum katika Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kufuatilia fedha zote zilizotolewa katika robo ya kwanza ya mwaka 2021.

Ripoti hiyo ya CAG inatarajiwa kuwasilishwa bungeni na kuwa wazi kwa umma wiki hii, ikigusa maeneo mengi ukiwamo ukusanyaji wa kodi kutoka vyanzo mbalimbali, uandaaji na utekelezaji wa bajeti ya serikali, hali ya Deni la Taifa, usimamizi wa rasilimali watu, usimamizi wa mali na madeni ya serikali, na usimamizi na uendeshaji wa taasisi za umma.

Vilevile, ripoti hiyo inatarajiwa kuangazia hali ya nguvukazi katika utumishi wa umma kwa maana ya uhaba wa watumishi, ujira na mafao yao kwa tafsiri yake pana pamoja na ukaguzi maalum uliofanyika katika maeneo mahususi.

Nipashe tunampongeza Rais Samia kwa hatua alizoanza nazo katika kuifanyia kazi ripoti hiyo. Ingawa hakuweka wazi sababu za kufanyika lwa uchunguzi BoT, kumekuwapo na madai kwamba baadhi ya vigogo walichota fedha kipindi ambacho Mkuu wa Nchi, Hayati Dk. Magufuli alikuwa mgonjwa.

Tunampongeza Rais Samia kwa kuchukua uamuzi huo kwa kuwa madai hayo ni mazito na ameonyesha mfano bora katika kuwajibika kwa umma na kiutendaji.

Ikumbukwe kwamba kila mwaka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) ambayo CAG ni mkuu wake, imekuwa ikiandaa ripoti kwa mujibu wa sheria na kuziwasilisha kwa mamlaka husika, lakini kilio kikuu cha CAG kimekuwa utekelezaji duni wa mapendekezo yake.


Mathalani, kuwapo kwa tatizo la watumishi hewa nchini kuliibuliwa kipindi cha uongozi wa CAG Ludovick Utouh, aliyeongoza ofisi hiyo kuanzia mwaka 2006 hadi 2014, lakini utekelezaji wa mapendekezo ya CAG kuhusu balaa hilo ulifanywa mwaka 2016, ukiwa ni mwaka wa kwanza madarakani kwa Hayati Dk. Magufuli.

Kwa kuzingatia kwamba ripoti za CAG huwa zinaandaliwa kwa weledi mkubwa na ndiyo jicho la serikali katika kufuatilia ufanisi wa kiutendaji, uwajibikaji na utawala bora, Nipashe hatutarajii kuona yale yaliyomulikwa na CAG, yanapokewa bila kufanyiwa kazi na mamlaka zinazohusika.

Tunafahamu kwamba ikishawasilishwa bungeni na mawaziri husika, Ripoti ya CAG itakabidhiwa kwa kamati mbili za Bunge zenye mamlaka ya kuifanyia uchambuzi ambazo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), lakini aliye na mamlaka ya kuchukua hatua kutatua ukakasi ulioripotiwa, ni serikali.

Kama serikali ikifumbia macho dosari zinazoibuliwa na CAG, ni wazi kwamba ripoti hizo za kitaalamu hazitakuwa na manufaa yoyote kwa taifa na hivyo kufifisha misingi ya uwajibikaji nchini. Shime, ripoti za CAG zifanyiwe kazi kuimarisha uwajibikaji kwa watendaji wa umma.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hapa pakiguswa vizuri, iko wazi patapunguzia elimu kero shuleni

**UAMUZI** wa serikali kuwapo elimu bure, umeleta unafuu kwa wazazi na walezi hasa kulingana na hali ya kiuchumi ya baadhi ya Watanzania, hatua inayochangia kuwapo tija katika sekta ya elimu, kwa kuwa inatoa fursa kwa kila mtoto kusoma.

Kimsingi, sera hiyo inamaanisha kufutwa kwa ada zote kuanzia elimu ya msingi hadi shule ya sekondari, ngazi ya kidato cha kwanza hadi cha nne. Wazazi wanakuwa huru kusomesha watoto wao katika ngazi hizo.

Pamoja na sera hiyo kuleta unafuu kwa wazazi na walezi, pia inatoa fursa kwa kila mtoto wa Kitanzania kupata elimu na imesababisha kero mbalimbali zinazochangiwa na baadhi kutafsiri vibaya sera hiyo.

Ni hali inayotokana na baadhi ya wazazi na walezi kuchagizwa na maneno ya baadhi ya wanasiasa majukwaani na hata wanaharakati ama kwa kudhania au kwa makusudi ya dhana zao, kwamba kupatikana elimu bora hakuna uhusiano na muungano wa majukumu na ushirikiano kati ya wazazi, serikali na wanafunzi.

Wapo wanaodhani kuwa, jukumu la kupata elimu kwa watoto wao ni la serikali peke yake, huku wao wakiwa na wajibu wa kufanya sehemu yao, kwamba ni njia ya kuboresha elimu nchini.

Hata ikiangaliwa kitaaluma na kiutawala, inapokuja suala la elimu bora, ni wazi linahitaji ushirikiano kati ya serikali, wazazi, wazazi na jamii kwa ujumla, pasipo kuisahau wadau wa elimu kitaifa.

Hivyo, inapendeza kushuhudiwa umma unaposhiriki kwa ujumla, kuwawezesha watoto wapate elimu bora.

Mfano hai, ni pale tangu sera ya elimu bila malipo ni mwongozo wa kisera ambao ulianza kutumika rasmi mwaka 2016, katika awamu ya pili ya uongozi wa nchi.

Sasa katika nyendo za utekelezaji na tafsiri yake ndiko kuna utata. Wako baadhi ya wazazi na walezi wanadiriki hata kugoma kuchangia chakula kwa ajili ya watoto shuleni, wakidai serikali ilishatangaza kutoa elimu bure.

Ni vyema tukakumbuka, serikali imeshatimiza wajibu wake wa kisera, ili kuwapa unafuu wazazi na walezi, pia wao wazazi na jamii hawana budi kutambua kuwa wana sehemu ya kufanya ikiwamo kuchangia chakula, ni njia mojawapo ya kuboresha elimu.

Binafsi ninaamini kuwa, iwapo kila mzazi atafanya sehemu yake, kero kwenye sekta ya elimu zinaweza kupungua, kwani pamoja na hatua ya serikali kuwa na sera ya elimu bila malipo, bado shule zinakabiliwa na kero mbalimbali.

Kutokana na kuwapo uhaba wa miundombinu hiyo katika shule mbalimbali nchini, ingekuwa vyema serikali ikaruhusu kuwapo michango midogo itakayoridhiwa na wazazi na walezi.

Yawekwe mazingira ambayo yatafanyika michango hiyo, isiwe ya lazima kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, bali ifanywe kwa utaratibu utakaoridhiwa na wadau wa elimu, wakiwamo wazazi wenyewe.

Wakuu wa shule, kamati na bodi wanaweza kuibua hoja hiyo na kuwashawishi wazazi na wadau wengine wa elimu, ili kuona umuhimu wa kuwapo kwa michango shuleni ambayo haiwaumizi.

Njia hiyo inaweza kuwasaidia wazazi na walezi kutambua na kutimiza wajibu wao kuwa wana sehemu ya kufanya wakati huu wa elimu bila malipo, ili kupunguza kero mbalimbali zinazozikabili shule za msingi na sekondari.

Iwapo hali itaendelea kuwa kama ilivyo sasa, si vibaya serikali ikaboresha sera hiyo ili kutatua kero zinazozikabili shule za msingi na sekondari wakati huu ambao elimu bila malipo inaendelea kutolewa,

Serikali inaweza kuelekeza fedha katika ujenzi wa madarasa, utengenezaji madawati ya kutosha na uboreshaji wa miundombinu mengine ya shule.

Ikumbukwe kuwa, hadi sasa wanafunzi wanaochaguliwa kuanza elimu ya kidato cha kwanza wamekuwa wakianza masomo kwa awamu kutokana na uhaba wa madarasa na wengine wanajikuta wakikaa chini kutokana na uhaba wa madawati.

Upo mfano kwamba, jumla ya wanafunzi 759,706 sawa na asilimia 91.1 ya wanafunzi waliofaulu wakiwamo wavulana 368,174 na wasichana 391,532 walichaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha kwanza mwaka 2021.

Hata hivyo, kuna wanafunzi 74,166 sawa na asilimia 8.9 wakiwamo wavulana 34,861 na wasichana 39,305 hawakupangiwa shule katika awamu ya kwanza, kutokana na uhaba wa madarasa.

## HABARI KITAIFA

# DC awachachamalia wazazi wasiochangia chakula shuleni

**Na Said Hamdani,** LINDI.

MKUU wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, amewaagiza watendaji wa vijiji, kata na tarafa kumpelekea ofisini kwake majina ya wazazi na walezi wanaokataa kuchangia chakula shuleni kwa ajili ya watoto wao wanaosoma shule mbalimbali za msingi.

Ndemanga alitoa agizo hilo,alipokuwa anazungumza na wakazi wa Kijiji cha Nandambi katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ,wakati wa ziara yake ya kukagua na kuhimiza shughuli za maendeleo zinazofanywa na jamii.

Alitoa agizo hilo, kufuatia uwapo wa taarifa kwamba baadhi ya wazazi na walezi wanadaiwa hawataki kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao wanaosoma katika shule mbalimbali za msingi ndani ya wilaya hiyo.

Ndemanga akizungumza na wakazi wa kijiji hicho Kata ya Chikonji, alisema anachukizwa na tabia ya baadhi ya wazazi na walezi wanaokataa kuchangia chakula kwa ajili ya kula watoto wao wanaosoma.

Amesema serikali imefanya mambo mengi, ikiwamo kuondoa malipo ya ada shuleni , lengo kubwa likiwa ni kuwapunguzia wazazi na walezi mzigo waliokuwa nao, lakini masuala ya chakula, sare na matibabu ni jukumu la wazazi.

"Serikali kwa upande wake imejitahidi ikiwamo kufuta ada na michangoili kuwapunguzia wazazi mzigo, hivi mnafikiri ifanye kitu gani tena?" alihoji Ndemanga.

Mkuu huyo wa Wilaya aliwaeleza wazazi na walezi walio na watoto wanaosoma na hawataki kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao kuwa hawatawafumbia macho badala yake watafikishwa mahakamani kujibu mashtaka.

Wakiunga mkono agizo la kiongozi huyo, wanafunzi Modesta Raphael, Juma Abdulli, Mwanaidi Said na Rehema, wanaosoma Shule ya Msingi Nandambi, walimshukuru wakisema mtoto anaposoma akiwa ameshiba, anakuwa na usikilizaji mzuri wa kile anachofundishwa na walimu wake.

Pia, walisema wanafunzi wanaposoma wakiwa na njaa inakuwa vigumu kushika na kuelewa kile anachofundishwa na walimu wao, na kwamba baada ya muda wanajikuta wakifanya vibaya katika mtihani ya Taifa.

# Bagamoyo waiomba TARURA kuweka mifereji barabarani

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO



Waziri wa Nchi , Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.

WAKAZI wa Kitongoji cha Tandika, Kata ya Kisutu Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani, wameomba Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kuhakikisha wanaweka mifereji kwenye barabara wanazotengeneza.

Wamesema wametoa ombi hilo ili kuondoa adha ambayo wamekuwa wakikumbana nayo, hasa kipindi cha mvua.

Wakizungumza jana katika kitongoji cha Tandika, walisema kukosekana kwa mifereji kumekuwa kukisababisha maji kuelekea kwenye makazi yaliyo karibu na barabara hizo.

Juma Ramadhani na Rajabu Issa walisema maji hayo yamekuwa yakiharibu nyumba zao na wengine kushindwa kuendelea na ujenzi licha ya kujaribu kuyawekea mwelekeo.

Ramadhani aliwaomba TARURA kufanyia kazi malalamiko hayo ambayo yamekuwa yakiwaumiza walio wengi hususani wanaoishi pembezoni mwa barabara hizo.

"Nimelazimika kutumia gharama zangu kujenga mfereji pembeni mwa nyumba yangu ili maji yasilete uharibifu, ninachoomba hawa TARURA watengeneze mifereji kwenye hizi barabara wanazojenga kuepusha madhara ambayo yanaweza kutokea," alisema Rajabu.

Walieleza kuwa nyumba zao ambazo zipo pembezoni mwa barabara mvua inaponyesha mvua kubwa maji yote yanajaa kwenye nyumba hizo, hivyo kuleta hofu ya makazi yao kusombwa na kukosa mahali pa kuishi.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**ISO 9001:2015 CERTIFIED**

## TAARIFA KWA UMMA

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Mdhibiti wa Sekta ya Mawasiliano ya Kieletroniki na Posta nchini. Pamoja na mambo mengine, ina jukumu la kusimamia gharama na tozo katika huduma za mawasiliano zinazotolewa na Watoa huduma na kuwalinda watumiaji wa huduma hizo.

Mnamo tarehe 5 Februari, 2021, TCRA ilitoa tangazo la kukaribisha maoni ya wadau kuhusu huduma za vifurushi zinazotolewa na Watoa huduma za mawasiliano ya simu za mikononi.

Kutokana na maoni hayo, TCRA iliandaa Kanuni ndogo za Vifurushi (Rules) za mwaka 2021, zenye lengo la kuweka utaratibu kwa Watoa huduma wa namna ya kupanga vifurushi, bei na muda wa matumizi ya vifurushi hivyo. Kanuni hizo zimeanza kutumika tarehe 02 Aprili, 2021.

Katika utekelezaji wa Kanuni hizi, watoa huduma waliwasilisha idadi na bei ya vifurushi vipya pamoja na bei za huduma nje ya vifurushi. TCRA imeidhinisha idadi ya vifurushi vilivyowasilishwa pamoja na bei za huduma nje ya vifurushi na tayari zimeanza kutumika tarehe 02 Aprili 2021.

Hata hivyo, TCRA imesitisha kwa muda matumizi ya bei mpya ya vifurushi vya data ili kutoa nafasi kwa Watoa huduma kupanga upya bei za vifurushi kwa ufanisi na kufanya uchambuzi wa kina kwa ajili ya kulinda maslahi ya watumiaji.

TCRA itaendelea kusimamia na kufuatilia kwa ukaribu huduma za mawasiliano kwa ustawi na maendeleo ya Taifa.

**IMETOLEWA NA MKURUGENZI MKUU**
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
**Tarehe 02 Aprili, 2021**

## Wakulima vitunguu walia ugonjwa kaukau

**Na Halfani Chusi**

WAKULIMA wa zao la kitunguu mkoani Iringa Wilaya ya Kilolo, Kata ya Ruaha Mbuyuni, wameiomba serikali kutafuta wataalamu watakaokuja na suluhu ya ugonjwa wa kaukau baada ya ugonjwa huo kudaiwa kuwa hatari zaidi kwa zao hilo na hauna dawa.

Hatua hiyo imekuja baada ya zaidi ya hekta 17 za kitunguu kuathiriwa na ugonjwa huo licha ya juhudi za wakulima kutumia kila aina ya dawa na kushindwa kupatikana suluhu.

Bwana shamba katika kata hiyo, Juma Shabani, ameliambia Nipashe kwa njia ya simu kuwa wamejitahidi kadri ya uwezo wao, lakini wameshindwa kupata suluhu na badala yake wameiomba serikali kuingilia kati kuleta wataalam.

"Ugonjwa huu wa kaukau umekuwa tishio sana kwa zao hili la kitunguu mwaka huu, kila kona kwa wakulima, hapa Ruaha Mbuyuni ni hichohicho watu wamewekeza katika ardhi, lakini wameambulia patupu," alisema.

Alisema zaidi ya hekta 17 mwaka huu zimekumbwa na janga hilo na ugonjwa huo unasambaa kwa kasi zaidi na baadaye utakuwa janga la nchi nzima kwa wakulima wa kitunguu na kwamba jitihada za lazima zinahitajika kutoka kwa serikali ili kuwakomboa wakulima.

Aliongeza walishapeleka sampuli katika vyuo vya utafiti (SUA) na Uyole vilivyopo Mbeya kwa muda mrefu, lakini bado hawajarejesha majibu kujua ni dawa gani ya kutumia.

Kwa upande wake, fundi pikipiki katika kata ya Ruaha Mbuyuni, ambaye pia ni mwathirika katika janga hilo, Maonezi Mohamedi, ameiomba serikali kuongeza jitihada za kuwanusuru wakulima hasa wanapoanza msimu mpya wa kilimo.

"Kwa sasa tunaanza msimu mpya tena wa kilimo na wakulima wamekata tamaa kwa kuhofia ugonjwa huo korofi shambani maana kama mwaka jana nililima heka tano sijaambulia chochote baada ya kuingiliwa na ugonjwa huo," alilalamika.

Naye Halima Ngambi, mkulima katika kata hiyo, alisema ugonjwa ulipoingia ulikuwa hauna madhara makubwa sana, lakini kwa sasa umekuwa na madhara makubwa.

# NEMC yanena siku 2 kabla ya ukomo mifuko ya plastiki

**Na Christina Mwakangale**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewakumbusha watumiaji wa mifuko ya plastiki kwamba, mwisho wa matumizi hayo ni Aprili 8, mwaka huu.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, akizungumza na Nipashe jana, alisema kama ilivyotangazwa awali na baraza hilo kuhusu ukomo wa matumizi ya mifuko hiyo, ni vyema jamii ikaanza kutumia vifungashio mbadala.

Machi mwaka huu, Dk. Gwamaka akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, alisema hakutaongezwa muda wa kusitisha matumizi ya mifuko hiyo kutokana na awali kuchukuliwa hatua kama hiyo.

Dk. Gwamaka alibainisha kwamba, kwa ambao watakiuka katazo la matumizi ya mifuko hiyo, adhabu yake ni pamoja na faini ya kuanzia Sh. 30,000 hadi 200,000 kutegemeana na kosa.

Pia, alisema kuwa wazalishaji wakubwa wa bidhaa za vifungashio vya plastiki ikiwamo viwandani adhabu ni faini ya Sh. milioni tano hadi Sh. Bil. 10 kutegemeana na aina au ukubwa wa kosa.

"Desemba 31, mwaka jana, NEMC, tulikumbusha kuhusu kanuni kwamba ilisema vifungashio ambavyo havijakidhi vigezo visionekane katika mazingira. Ili kwa wanaotumia vifungashio na kutengeneza kwa wingi wasajiliwe au kupewa maelekezo," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema lengo la kanuni na katazo hilo ni kulinda mazingira na kuwa endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Dk. Gwamaka alisema kanuni iliwekwa ili kulinda mazingira, kupunguza uchafuzi kutokana na mifuko ya plastiki ambayo haiozi ardhini kwa takribani miaka 400 hadi 500.

"Tusiishi kama sisi ndio kizazi cha mwisho katika hii dunia, kwa kuchafua mazingira kana kwamba hakuna viumbe wengine baada ya kizazi hiki, tumeikuta ardhi safi na sisi tunaiacha chafu, si sahihi," alisema Dk. Mafwenga.

Alisema wanaozalisha vifungashio wana wajibu wa kuzirejesha bidhaa zao viwandani ili kulinda mazingira na kwamba wajasiriamali na wafanyabiashara wageukie matumizi ya mifuko ya karatasi na katani kwa kuwa kuna viwanda vinavyozalisha nchini.

"Tarehe 8, Januari mwaka huu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, alionyesha huruma na kuongeza muda wa matumizi ya mifuko hii, sheria inakataza ndio maana wakapewa miezi mitatu, kusiwe na bidhaa ambayo TBS (Shirika la Viwango Tanzania) haijaruhusu, haijasajiliwa na kuwa sokoni.

Kadhalika, Dk. Gwamaka aliwataka wenye viwanda na wajasirimali wa bidhaa za vyakula, mifugo na kilimo kuanza kujiandaa kutumia vifungashio mbadala rafiki wa mazingira, ili kuepuka adhabu.

"Muda huo ukifika hatutarajii walio na viwanda kuona kama tunawaonea ndio maana tunaawarifu mwezi mmoja umebaki, matumizi ya mifuko hii, iwe ni wauza miwa, yeyote, wajipange," alisema Dk. Gwamaka.




Binti akisaidia mzee mwenye ulemavu wa kuona, kuomba msaada kwa abiria wa daladala, eneo la Mwenge jijini Dar es Salaam juzi. Ingawa kumekuwapo na jitihada za kuwaondoa ombaomba mitaani, bado hazijazaa matunda. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mch. ataka maombi zaidi kuiombea serikali

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MCHUNGAJI wa Kanisa Anglikana la Mtakatifu Gabriel Kibaha mkoani Pwani, Exavia Mpambichile, amewataka waumini wa kanisa hilo na Watanzania kwa ujumla kuendelea kufanya maombi kwa ajili ya serikali hasa wakati huu ambao mabadiliko mbalimbali ya viongozi wa ngazi za juu yanaendelea ili yafanyike kwa amani.

Aliyasema hayo juzi wakati akitoa mahubiri yake kwenye ibada ya Pasaka katika kanisa hilo ambapo alisema kuwa utamaduni wa Watanzania ni wapenda amani ambayo ndio msingi wa maendeleo hivyo ni vema wajitahidi kuilinda na kusimama kwenye maombi.

Alisema kuwa ili viongozi waendelee kufanya kazi kwa kufuata kanuni na kujali maslahi ya wengi kuna ulazima wa Watanzania kuwaweka kwenye maombi kila siku bila kuchoka kwani kazi wanayoifanya ni kubwa.

Aliwataka waumini hao kutotumia Sikukuu ya Pasaka kinyume cha kanuni za Mungu hasa kujiingiza kwenye vitendo viovu kwani kufanya hivyo ni kujiweka kwenye mazingira hatari ambayo hasara yake ni kubwa.

HABARI KITAIFA

# RC aagiza ukaguzi ujenzi nyumba ya jaji

**Na Tigana Vincent,** TABORA

KATIBU Tawala Mkoa wa Tabora ametakiwa kupeleka Wataalamu wa ukaguzi kutoka maeneo mbalimbali kwenda kufanya ukaguzi kwenye mradi wa ujenzi wa nyumba ya Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora ili kujiridhisha kama fedha zilizoshatumika zinalingana na kazi zilizofanyika.

Hatua inayofuatia nyumba hiyo kujengwa kwa zaidi ya miaka 10 na kugharimu fedha nyingi wakati Jaji Mfawidhi akiendelea kuishi katika nyumba ya kupanga.

Agizo hilo lilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Tabora , Dk. Philemon Sengati (pichani), alipotembelea kuona hatua ilipofikia nyumba ya kiongozi huyo, baada ya uongozi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora kumwomba kuwasaidia kusukuma mbele suala hilo.

Alisema hadi hivi sasa nyumba hiyo imegharimu Sh. milioni 405, lakini bado kazi nyingine kama kuunganisha maji, kujenga kibanda cha walinzi na kukamilisha uzio hazijakamilika.

Dk. Sengati alisema licha ya Serikali kuvunja mkataba na kampuni ya ukandarasi ya Nice Standard Investment Ltd ya Dar es Salaam mwaka 2014 kwa sababu ya kazi kwenda polepole na kukabidhi kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) bado kazi inaendelea kusuasua.

Alisema kitendo cha kuendelea kuichelewesha kumesababisha baadhi ya maeneo kuanza kuchakaa na kitaiongezea serikali gharama mpya na kuwataka TBA kuwa wazalendo wanapopewa kazi

Naye Mtendaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Cosmas Lugora, alisema mahakama imekuwa ikitumia fedha nyingi kulipia pango la nyumba ya Jaji Mfawidhi kila mwezi wanalipa Sh. milioni moja.

Alisema tangu mwaka 2010 ambapo nyumba ndipo ilipotakiwa kukamilika, wametumia fedha nyingi ambazo zingesaidia kuboresha huduma nyingine za utoaji wa haki kwa wananchi.



Lugora alisema kila mwaka wamekuwa wakiwasiliana na TBA na kupewa ahadi ambazo hawazitimizi na kumuomba Mkuu wa Mkoa awasaidie kuuhimiza wakala huo kumalizia nyumba hiyo ili Jaji Mfawaidhi aweze kupata sehemu nzuri ya kuishi na kutekeleza majukumu yake vema.

Kaimu Meneja wa TBA Mkoa wa Tabora, Abraham Ndazi, alisema ujenzi ulisimama tangu Novemba 2017, kutokana na ukosefu wa fedha za kumalizia kazi zilizobaki.

Alisema wamekwishapeleka maombi ya Sh. milioni 204.9 za kumalizia kazi mbalimbali zilizobaki.

# Waguswa na ujenzi wa SGR

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI wa Malampaka, wilayani Maswa mkoani Simiyu, wameeleza faida za mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR Sehemu ya tano itakayojengwa kutoka Mwanza hadi Isaka KM 349 ikiwamo upatikanaji wa ajira na ukuaji wa uchumi.

Akizungumza mbele ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Dk. Leonard Chamuriho, Juma Saidi alisema wako tayari kushiriki kwenye mradi na kuahidi kulinda vifaa vitakavyotumika kwenye ujenzi.

"Sisi tumeshajipanga kufanya kazi sababu tumeshaona vifaa vimewasili, tuko tayari kufanya kazi kwa bidii ili tupate kipato lakini pia tushiriki moja kwa moja kutimiza historia ya nchi kupitia mradi huu," alisema Mzee Saidi.

Waziri Dk. Chamuriho alisema Serikali imeridhishwa na matayarisho ya mkandarasi kwani ameshaanisha maeneo ya kuweka kambi, eneo la kuchimba kokoto, kuwasilisha vifaa pamoja na kukamilisha reli ya mfano.

"Kama mnavyoona mkadarasi yuko kwenye eneo la ujenzi na sehemu kubwa ya maandalizi imekamilika ikiwamo mitambo, hapa kitakachofuata ni kumpa taarifa mheshimiwa Rais Samia Suluhu ili kuweka jiwe la msingi na ujenzi kuendelea," amesema Waziri Chamriho.

Waziri Chamriho alisema Wizara itaendelea kusimamia kwa karibu miradi yote ya sekta ili ikamilike kwa ubora na wakati na kuwaomba wananchi kujipanga kutumia fursa hiyo kujiimarisha kiuchumi.

Aidha, Waziri Chamriho alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Juma Sweda, kwa kusimamia uhamasishaji wananchi kupisha kwenye maeneo ambayo reli itapita na kuwaahidi wananchi hao kuthamini utakapokamilika watalipwa fedha zao.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, aliwataka wananchi na wakazi wa Mwanza na Simiyu watakaopata kazi kwenye mradi huo kujiepusha na wizi wa vifaa na mafuta ili kufanya mradi huo kukamilika kwa wakati.

"Katika sehemu nyingine kwenye ujenzi wa mradi huu kumetokea vitendo vya wizi sasa niwahakikishie serikali haitamvumilia mwananchi yoyote atakayekamatwa na kifaa chochote kitakachokuwa kwenye mradi huu" alisisitiza Naibu Waitara.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Misungwi, Juma Sweda, aliishukuru serikali kwa kuendelea kutekeleza mradi huo mkubwa wa kitaifa na kumuahidi Waziri na Naibu Waziri kuwa wataimarisha ulinzi ili kufanikisha mradi huo.

Mradi huo unaanzia Dar es Salaam hadi Mwanza (KM 1,219), umegawanyika katika sehemu tano ambazo ni Dar es Salaam mpaka Morogoro, Morogoro mpaka Makutupora, Makutupora hadi Tabora, Tabora hadi Isaka na sehemu ya tano ni Isaka mpaka Mwanza inayojengwa na kampuni ya China Civil Engineering Consruction Corporation (CCECC-CRCC) ambayo Mkataba wake ulisainiwa mwezi Januari, mwaka huu.



# Moro walivyomwombea Magufuli

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WANANCHI na viongozi mbalimbali wakiwamo wa serikali, siasa na kidini wameshiriki katika ibada maalumu ya kumwombea Hayati Dk. John Magufuli, huku Kiongozi Mkuu wa Huduma ya Sauti ya Uponyaji Tanzania, Nabii Joshua Ararm Mwantyala, akimweleza Dk. Magufuli ndie rais aliyeonyesha njia kwa Watanzania.

Aidha, kiongozi huyo wa kiroho alisema Hayati Dk. Magufuli licha ya kuwaonyesha njia Watanzania, pia amehakikisha Tanzania inapaa kimaendeleo katika nyanja na kufikia uchumi wa kati kwa kutumia fursa mbalimbali zikiwamo za kiuchumi .

Akizungumza katika ibada hiyo maalumu iliyoandaliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro na kufanyika katika Uwanja wa Jamhuri, Nabii Joshua alisema alikuwa akimtanguliza Mwenyezi Mungu mbele, na kuwa Hayati Dk. Magufuli alipambana na rushwa, kutetea wanyonge, ikiwamo kuanzisha miradi mingi ya kimaendeleo.

Aliongeza kwamba anaamini kuwa Rais Samia Suluhu Hassan akimtanguliza Mwenyezi Mungu mbele, Taifa hili litapiga hatua kubwa na kusonga mbele.

Nabii Joshua alimtaja Hayati Dk. Magufuli alikuwa 'jembe' la nguvu na Serikali yake ikajizatiti kutoa elimu bila malipo kuanzia shule ya msingi hadi sekondari na kufuta michango iliyokuwa inawanyanyasa wanyonge.

"Wakati wa uhai Hayati Rais Dk. Magufuli alitueleza kwamba kwa njia ya elimu makini, hata watoto wa Watanzania maskini wataweza kutoboa na hatimaye kupata maisha bora zaidi, jambo ambalo linatokana na ukweli kwamba elimu ni ufunguo wa maisha," alisema Nabii Joshua.

Aliyataja baadhi ya mafanikio hayo kwenye uongozi wa Serikali ya awamu ya tano chini ya Hayati Dk. Magufuli, iliweza kujenga zahanati 1,198, vituo vya afya 497 na hospitali za wilaya 71.

Nabii Joshua, alisema Dk. Magufuli alitambua kwamba, afya bora kwa Watanzania ni mtaji katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo fungamani ya binadamu.

Aliwataka Watanzania kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa maisha ya Hayati Dk. Magufuli na kuwataka wayashangilie maisha yake kwani kazi aliyoifanya kwa kipindi cha miaka sita ya uongozi ni kazi ambayo inapaswa kuienzi kwa kumshukuru Mungu kwa zawadi hiyo kwani inawezekana kuwa Mungu alimchukua kwa kufanya alama yake isifutike .

Kwa upande wake Katibu wa CCM Mkoa wa Morogoro, Alexandria Katabi, alisema hayati Dk Magufuli katika uhai wake alikuwa na nia ya dhati ya kukuza uchumi na kuiletea Tanzania maendeleo.

Katabi alisema Dk. Magufuli amefariki, huku nyuma akiacha miradi mikubwa ya kimaendeleo ambayo ikikamilika itaiweka Tanzania katika ramani ya viwango vya juu vya maendeleo .

" Tumeamua kufanya Ibada hii kwa Hayati Rais wetu Dk. Magufuli, kutokana na mema yake aliotufanyia katika Taifa hili pamoja na kuwombea Rais Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ili waweze kuongoza nchi vyema katika kipindi hiki kigumu cha majozi," alisema Katabi.

Viongozi mbalimbali wa dini waliOshiriki katika kumwombea hayati Dk. Magufuli wakiwamo kutoka Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA) Mkoa wa Morogoro, Kanisa la Kiinjili la Kilitheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Morogoro, Kanisa Katoliki Jimbo la Morogoro na Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Morogoro.



Baba lishe, Fabian Ezekiel, akiandaa chakula aina ya ugali katika Soko la Kariakoo jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kuwauzia wateja.
**PICHA: JUMANNE JUMA**

## Wamlilia mbunge wao awatengenezee barabara

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKAZI wa vijiji vya Uzogole na Bugwandege Kata ya Ibadakuli Manispaa ya Shinyanga, wameingiwa na hofu ya kusombwa na maji baada ya barabara inayounganisha vijiji hivyo viwili kukatika.

Walipaza kilio hicho jana wakati Mbunge wa Jimbo la Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi, alipofanya ziara kujionea ubovu wa miundombinu ya barabara kwenye eneo hilo la Kata ya Ibadakuli na kusikiliza kero za wananchi.

Mmoja wa wananchi hao, Charles Nyuma, alisema barabara hiyo ilikatika tangu Novemba mwaka jana, lakini bado wanaendelea kuvuka hivyo hivyo pamoja na wanafunzi na kuhofia kwamba ipo siku yatatokea maafa kwa kusombwa na maji.

"Tunaiomba Serikali itutatulie changamoto hii ya kukatika kwa barabara sababu ya mvua, na ni kiunganishi katika vijiji viwili na kuna shule, ambapo watoto wetu wanavuka... pia kwenye haya maji na ni hatari kusombwa na maji," alisema Nyuma.

Naye Elizabeth Robert, alisema kukatika kwa barabara hiyo kunawafanya washindwe kupeleka watoto wao klinikia na hata kufanya shughuli zao za kiuchumi, na kuomba ifanyiwe matengenezo haraka.

Kwa upande wake Naibu Meya wa Manispaa ya Shinyanga, David Nkulila, alisema Serikali itatuma wataalamu kwenda kufanya usanifu wa kina, ili kubaini bajeti na kuitengeneza barabara hiyo.

Mbunge Katambi, ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana na Ajira), alisema kwa sasa wanakwenda kwenye Bunge la Bajeti, na kuahidi kusimamia matengezo ya barabara hiyo.

Pia alitoa wito kwa wananchi wachukue tahadhari wakati wa uvukaji wa barabara hiyo, na hasa kuacha kupita pale maji yanapokuwa yamejaa ili kuepuka kusombwa na maji na kutokea maafa.

# Watakiwa kujenga vyumba vya madarasa ya ghorofa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga imewaagiza walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari za Halmashauri za Ushetu, Manispaa ya Kahama Mjini na Msalala kujenga vyumba vya madarasa vya ghorofa ili kubana matumizi ya ardhi kutokana na baadhi ya shule kuwa na uhaba wa maeneo.

Anamringi Macha, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, aliyabainisha hayo juzi wakati wa hafla maalumu ya kupokea mifuko 50 ya saruji yenye thamani ya Sh.1,000,000 iliyotolewa na Kampuni ya Nyati Cement ambayo itagawanywa katika Shule ya Msingi Nyahanga na Kabalae.

Alisema kutokana na changamoto ya ufinyu wa maeneo ya shule katika shule za msingi na sekondari kuanzia mwaka 2022 wataanza ujenzi wa vyumba vya madarasa ya ghorofa hususani kwa shule za msingi zilizopo mjini ili kubana matumizi bora ya ardhi.

"Ninatoa maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri zote kuhakikisha wahandisi wa ujenzi wanawasilisha michoro ya vyumba vya madarasa vya ghorofa ofisini kwangu ili nikaiwasilishe serikalini.......Tusipoangalia maeneo ya shule yatakwisha kwa ujenzi holela ambao unachukua eneo kubwa," alisema Macha.

Pia Macha alisema wameamua kuanza ujenzi huo ili kunusuru shule nyingi za mjini kukosa maeneo kutokana na aina ya ujenzi unaoendelea kutumika wa msururu ambao umekuwa ukichukua eneo kubwa na kusababisha shule nyingi kushindwa kujengewa uzio.

Aliishukuru kampuni ya Nyati kwa kutoa mifuko 50 ya saruji ambayo itatumika kujenga vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Nyahanga Halmashauri ya Manispaa ya Kahama na Kabale Msalala ambapo kila shule itapatiwa mifuko 25.

Akikabidhi saruji hiyo kwa Mkuu wa Wilaya, Ofisa Uhusiano wa kampuni hiyo, Fadhiri Yustac alisema saruji hiyo imegharimu Sh.1,000,000 na wametoa ili kurudisha faida kwa wananchi kutokana na biashara wanayoifanya kanda ya ziwa kwa kiwango kikubwa.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Kabale, Elias Kihamba, alisema wana uhaba wa vyumba vya madarasa 40 na vilivyopo ni nane, kimoja kinatumiwa kama ofisi za walimu, huku idadi ya wanafunzi 1,268 wakitumia madarasa saba pekee.

Nipashe
# TESA
Jumanne Aprili 6, 2021
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14

**Namna halisi Kiswahili kinasuasua kutokana na kukinzana hoja tata**



Mila potofu inavyozalisha majanga, mkasa wa binti kuondolewa matiti



Ukurasa 13

TEKNOLOJIA
**NA BEATRICE SHAYO**

# Mama mwenye umri makamo aingia darasani, abobea teknolojia majiko

• Yamvusha kutoka 'hoi' hadi mwekezaji • Ana karakana, mshirika mkuu mumewe • Sokoni; hotipoti, chupa ya chai za udongo...

TABU Kashele, ni mwanamama mwenye umri wa miaka 65, ambaye ana watoto watano. Ana simulizi ya jinsi alivyokuwa akichekwa, pale alipokuwa anatafuta udongo kwa ajili ya kutengeneza majiko.

Hawakujua ni safari ya kiteknolojia, akitafuta malighafi udongo atimize ujuzi wake, ambao mbele unamfanikishia maisha.

Mama Tabu anasema, ni safari ya ujasiriamali ambayo amekutana na changamoto mbalimbali, haikuwa rahisi kutokana na wengine kumzungumzia umri wake umekwenda na kile anachokifanya katika kujitafutia kipato.

Anasema, hakuangalia vikwazo alivyokutana navyo ilikuwa ni kutimiza sura mbili za malengo, anatumikia ujuzi wa kiteknolojia aliyo nayo yenye dhamira ya kuhakikisha anatengeneza majiko bora, yatakayomwingizia kipato, akiwa na soko la ndani na nje ya nchi.

"Watu walikuwa wananicheka umri wangu ni mkubwa eti nacheza na udongo, mara nimekosa kazi za kufanya sikusikiliza maneno yao. Nilihakikisha natimiza kile ambacho nakitaka kukifanya hata kama umri wangu umeenda," anasema

### NI JIKO AINA GANI?

Tabu anasema jiko analotengeneza lina pembe nne na kando yake ina sehemu ya kutoa mvuke, kunakowekwa kuni moja hata mtu anaweza kupika chai kwa mvuke, unatengeneza vyakula kwa njia ya mvuke.

Anasema, jiko hilo halihamishiki na limekuwa likipendwa katika maeneo ya vyuo, tena lisilotumia gharama kubwa katika matumizi yake ya msingi.

Tabu anasema, kuna wakati ilimlazimu kujiongeza na kutengeneza majiko yanayohamishika, ili hata waliopo katika maeneo kama vile mikoa ya mbali wanakoweza kufaidika na huduma hiyo.

"Nilikaa chini nikajiuliza mtu ambaye yupo Shinyanga atawezaje kulinunua hili jiko? Ikabidi niwe mbunifu na kutengeneza majiko ambayo yanahamishika," anasimulia.

Mteknolojia huyo anasimulia kwamba, majiko yake anayatengeneza kwa kutumia udongo mfinyanzi na baada ya kukamilika, huyachoma na kuyaweka katika mwonekano bora.

Kuhusu namna alivyojisogeza katoka katika ujasiriamali wa kutengeneza majiko hayo, anasema alianza rasmi mwaka 1995 na jiko moja alianza kuuza kwa bei ya Sh. 500, lakini namna yalivyokuwa na mvuto kwa wateja alijikuta ana mauzo ya jumla ya Sh, 50,000, jambo lililomfurahisha maradufu.

### LINI WALIANZA?

Mama Tabu anasema ulikuwa mwaka 1992, walipohamasishwa kujifunza kutengeneza majiko yasiyohamishika kutoka kwa raia mmoja wa Kizungu, ambaye hamkumbuki jina lake, alikuwa mkazi wa jijini Mwanza.



Tabu Kashele akitengeneza chupa ya chai. **PICHA: BEATRICE SHAYO**

Katika mafunzo hayo ya mwaka 1992, anaeleza walipekekwa nchini Kenya kujifunza zaidi na kujionea jinsi watu wanavyotajirika kutokana na majiko aina hiyo ya udongo, jumla yao wakiwa wanafunzi 110.

Tabu anafafanua: "Alikuja Mzungu kuhamashisha yale majiko yasiyohamishika tukapelekwa Kenya kuona wenzetu walivyoendelea tulikuta watu wanatajirika kwa ajili ya udongo nilihamasika."

Anasimulia kwamba, ilichukua mwaka mmoja kwa mafunzo hayo kukamilika kwa kupatiwa cheti cha kutengeneza majiko, kazi aliyoendelea na shughuli zake za kutengeneza majiko mwaka 2013, alipata wafadhili wanaojulikana kutoka asasi kutoka nchini Canada aliyoitaja kuwa na ofisi mkoani Mwanza.

Tabu anaendeleza simulizi kwamba, baada ya kumuona anatumia nguvu kubwa katika utengenezaji majiko, alipatiwa vifaa vya mashine kwa ajili ya kurahisisha kazi yake, kwani awali alitumia mikono.

### ALIVYO SASA

Mama huyo anasema, kwa sasa naye ana mashine anayotengeneza kila siku majiko 100 na akishawafundisha wanafunzi

INAENDELEA UK.12

# Mama mwenye umri makamo aingia darasani, abobea teknolojia majiko



Bidhaa ambazo ni zao la ufundi wa Tabu Kashele.

**INATOKA UK.11**

149,000 katika maeneo anayoyataja kuwa ni Simiyu, Mwanza, Bariadi, Morogoro, Kahama pia nchi jirani, zikiwamo Rwanda, Burundi na Uganda.

Anasema, mbali na anaowataja kuna wanafunzi wanaoenda nyumbani kwake kujifunza, hali kadhalika wengine huwafuata katika mikoa waliopo na hadi sasa anaendelea na kazi anayotengeneza majiko aina ya matawi.

Mama huyo mtaalamu anasema, aina ya majiko hayo yamempa umaarufu, kwa siku anaweza kuyauza 10 hadi 20 na mengine wakala wake husambaza katika maeneo mbalimbali.

Anasimulia kuna wakati alipatiwa tuzo ya usafiri aina ya Bajaji kutoka kwa wafadhili ili kumwezesha kusambaza bidhaa zake kwa wakati.

Pia, anasimulia kwamba, kwenye maonyesho huwa anauza majiko mengi, kila moja akiuza kwa bei ya Sh. 6,000 na jiko lenye matawi makubwa bei yake inafikia Sh. 10,000, huku maalum anayoyajenga yanafika bei Sh. 20,000.

Kwa mujibu wa mteknolojia huyo, majiko hayo ni ya gharama nafuu zaidi, kwani mtu anatumia mkaa wa Sh. 1,000 kwa siku tatu.

Tabu anasema kwamba, mbali na kutengeneza majiko, pia kuna chupa za chai za udongo zinazotengezwa, inayotumia saa kadhaa pasipo kupooza chakula.

Mwanamke huyo anasema, mustakabali wa teknolojia hiyo inafika hatua za kuunda hotipoti, bakuli, vifaa vya kuwekea mishumaa kama umeme unapokatika na pasi inayotumia mikaa mitatu, vikombe vya chai ya udongo anavichoma haviwezi

> “Mume wangu alinipa ushirikiano mkubwa. Tulikuwa tunakwenda wote kuchimba udongo, kwa sasa hatuna shida tunajitosheleza sisi wenyewe.



Mtaalamu Tabu Kashele akiwa kazini. **PICHA ZOTE: BEATRICE SHAYO.**

kumong’onyoka.

**CHANGAMOTO JE?**

Mama huyo anataja upatikanaji wa masoko ni tatizo, akiongeza: “Kuna wateja wengine wanataka kazi na baada ya siku wanakaa kimya hiyo ni changamoto ambayo hainisumbui, nitapambana nitauza kwa wateja wengine.”

Anasema awali alivyokuwa anachimba udongo, ilikuwa bure na sasa walivyomuona udongo una faida, wakaanza kumuuzia.

**MAISHA YAKE?**

Tabu anasema biashara hiyo imemwezesha kupata mafanikio mbalimbali ikiwamo kumiliki nyumba mbili za kisasa.

Anasema awali alikuwa ni mama wa nyumbani na biashara hiyo aliianza akiwa ni mtu mzima na kuna watu walifikia hatua ya kumcheka pale alipoonekana akihangaika kubeba udongo ambao ndio malighafi yake .

Pia anataja katika harakati hizo wapo wengi walisoma pamoja katika darasa la teknolijia hiyo, lakini waliiona kazi hiyo ngumu, akajikuta amebaki peke yake aliyeenda kuanzisha mradi wa kutengeneza majiko.

Hata hivyo, anakiri kapitia hatua ngumu za kutetea teknolojia na maisha yake kiuchumi, huku akiitaja kuwa sababu mojawapo ya kung’ang’ania mwelekeo huo.

Mama huyo anarejea kwamba, akiwa katika hali ngumu ya kiuchumi aliyokuwa nayo, alipofika nchini Kenya alishuhudia namna wanufaika wa teknolojia hiyo ya udongo walivyonufaika.

Hapo katika kufanikisha anachokifanya sasa, anasema hivi sasa anashirikiana na mumewe aliyebeba jukumu la kuyang’arisha na kuyaweka imara majiko hayo anayotegeneza kwa udongo, baada ya kukauka kwa kuyarembesha na kisha anapeleka kuzichoma.

“Mume wangu alinipa ushirikiano mkubwa. Tulikuwa tunakwenda wote kuchimba udongo, kwa sasa hatuna shida tunajitosheleza sisi wenyewe. Hatupendi kuwasumbua watoto hata tunapokuwa na changamoto tunajitahidi kujisaidia,” anasema

Katika kuhitimisha hilo, wameajiri vijana kwa ajili ya uchimbaji udongo na kuponda, huku akiwa katika mchakato wa kujenga karakana ya kutengenezea majiko ya chuma.

Hadi sasa anajivuna mradi wa majiko umempa faida nyingine ya kuanzisha kilimo cha mpunga ekari saba na amenunua ng’ombe 12, pia mashamba kadhaa.

**WABUNIFU MRADI**

Meneja Miradi wa Mtandao wa Nishati na Jinsia Tanzania (TANGSEN), Thabit Mikidadi, anasema wana lengo la kuona wanawake wengi zaidi wanashiriki katika sekta ya nishati katika ngazi za uamuzi kama wafanyabiashara, vilevile katika ajira na fursa nyingine zinazojitokeza.

Anasema TANGSEN inawajengea uwezo wanawake, ili waweze kuitumia nishati hasa ya umeme katika kuzalisha majiko hayo, akifafanua kwamba wanawake wakiwa wengi katika ujasiriamali wa nishati, wanaongeza wigo wa uchumi na kuinua pato la familia.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Mila potofu inavyozalisha majanga, mkasa wa binti kuondolewa matiti

- Tendo lenye miaka 18, bado lamtesa
- Pia simulizi maziko yanabeba viulizo

HADI sasa kunatajwa kuwapo baadhi ya mila zinazoendelezwa barani Afrika zinawafanya kutambua urithi wao wa kiutamaduni.

Pia, kunatajwa baadhi ya mila zinazokiuka haki za kimsingi za binadamu, hata katika mtazamo kwamba katika baadhi yake, ni jambo la kawaida kwa jamii zinazofuata, kile ambacho kwa wengine huenda ni cha kushangaza.

Zipo mila zinapigwa vita ndani ya nchi husika kwa sheria zake na zingine kufikia kiwango cha kimataifa, katika mashirika mbalimbali kama vile Umoja wa Mataifa, zikipewa hadhi ya mila kandamizi, ambazo hazina nafasi tena katika karne iliyopo sasa.

Kumeshuhudiwa katika baadhi ya makabila, mathalan mojawapo la jamii la kifugaji, mazishi ya heshima kwa wazee wenye mchango wao ndani ya jamii umetambulika, anazikwa akiwa ameketi baada ya kufunikwa kwa ngozi ya ng'ombe.

Pia, kaburi la wazee hao huwa ni la duara, ujenzi wake unachukua miezi tisa, ikirejea tafsiri kwamba ni sawa na kipindi anachobeba mimba mwanamke hadi kujifungua. Imani iliyoko ni kwamba, mtu kama huyo hajafa bali atazaliwa tena.

Ni nani anazikwa hivyo katika kundi la watu maarufu, wazee wa jamii husika ndio wanaamua anayestahili kufanyiwa hivyo ya heshima, baada ya kufanya tathmini.

### MAZIKO YA USIKU

Katika jamii ya Zulu nchini Afrika Kusini na badhi ya sehemu nyinginezo za Afrika, Mfalme akifariki huzikwa wakati wa usiku katika mazishi yanayohudhuriwa na wanaume pekee, mfano hai ukiwa ni wa Mfalme Goodwill Zwelithini, aliyezikwa siku chache zilizopita baada ya kuaga dunia kutokana na virusi vya corona .

Waziri Mkuu wa Kitamaduni wa Prince Mangosuthu, Buthelezi, anasema mfalme huyo angezikwa katika hafla ya kibinafsi wakati wa usiku, ikiwa ni sehemu ya mila na desturi za jamii ya kabia la Wazulu .

Katika mazishi hayo, ni kundi maalum la wanaume kutoka nyumba ya kifalme ya Zulu, ndio wanaoruhusiwa kushiriki.

### HOFU YA LAANA

Magharibi mwa nchini Kenya, kuliripotiwa dai la hofu ya laana, wazee kutoka jamii la kabila la Wabukusu waliamua kwenda kuifukua baadhi ya miili ya wapendwa wao na kuizika kwa wanachokiona 'njia inayofaa' kwa katika utamaduni wao .

Inadaiwa kuwa, desturi za jamii hiyo ni kwamba kichwa cha mfu kinafaa kuangalia upande usionendana na mwelekeo wa boma lao, mavazi kama viatu, shati, au tai vinafaa kulegezwa katika mwili wa marehemu.

Ni hatua iliyochukuliwa, kupingana na namna maziko yalivyofanywa na maofisa wa afya, kwani wanadiwa waliaga dunia kutokana na maradhi ya corona na jamaa za walioaga dunia kuikaribia miili ya wapendwa wao wakati wa maziko hayo.

Wazee wa jamii hiyo walisema iwapo hilo halingefanyika inaaminika mtu aliyefariki anaweza kuitesa familia yake katika ndoto zao.



Watu wakiwa katika nyendo za kimila. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



### 'PASI' ZA MATITI'

Katika Afrika Magharibi na hasa nchini Cameroon, utamaduni au mtindo wa 'kupiga matiti pasi' kuyazuia yasiwe makubwa umekithiri

Wanaotekeleza hayo wanadai kwamba hatua ya kuzuia kukua matiti ya wasichana wanaoanza kuvunja ungo, wanazuiwa kuwavutia wanaume, hivyo wanaepuka dhuluma za kimapenzi, lakini ni jambo lialotajwa na wanaharakati kama ukiukaji wa haki za wasichana na dhuluma za kijinsia .

Inafanyikaje? Hapo jiwe hutiwa katika moto na kisha jiwe hilo linapitishwa juu ya matiti, kwa lengo la kuyapunguza ukuaji wake.

Hapo kuna ushuhuda wa msichana, aliyefanyiwa tendo la utamaduni na shangazi yake, miaka 18 iliyopita aliyekuwa mtawa akiishi nchini Cameroon wakati huo.

Binti huyo anasimulia kwamba, shangazi huyo alipofika nyumbani kwao likizo wakati huo, alimkuta kishavunja ungo na matiti yake yalikuwa yameanza kujitokeza na kuonekana kupitia nguo yake.

Shangazi yake hakufurahia hilo na mara moja akamwambia mama wa binti huyo, kwamba mwana huyo yuko hatarini kubakwa na wanaume, hivyo kulikuwapo haja ya kuyapunguza matiti yake.

Mama yake alishangaa uwezekano wa kufanyika hilo, lakini shangazi yake kwa ajili ya kuwa mtawa aliheshimiwa sana pale bomani aliko, uamuzi wake ulibeba sura ya sheria.

Mtawa huyo alieleza jinsi utaratibu huo ungefanywa na muda ulifayika kikatili, huku mtendewa binti huyo alivumilia takriban dakika 20 za uchungu, wakati jiwe la moto lilipokuwa likiwekwa kifuani mwake kupunguza ukubwa wa matiti yake.

Alipofika shuleni, wenzake walishangaa, mbona alikuwa akilia wakati wote na kushika kifua chake kwa uchungu. Pia, rafiki zake wa karibu walishangaa mbona hawakuwa wakioga pamoja kama awali, bila kujua mwenzao alikuwa akificha alama aliyo nayo kifuani.

Hali ya matiti yake kupungua kutokana na uovu aliyokuwa akifanyiwa na shangazi yake, ni sehemu ya mila aliyoitoa Cameroon.

Alipokuwa msichana mkubwa ngazi ya kujiunga na elimu ya chuo kikuu, binti huyo alikutana na matatizo makubwa ya kisaikolojia kuhusiana na hali ya kujiamini, kwa sababu alijihisi tofauti, hasa pale alipojilinganisha na wasichana wenzake.

Wengine walikuwa wandiriki kumfanyia mzaha, kwa kumuita 'mvulana' kwa sababu alikosa matiti bila ya kujua masahibu aliyopitia.

Binti huyo hakuweza kumchukulia hatua yoyote ya kisheria shangazi yake, kwa sababu uamuzi huo alihisi pia ungemuingiza hatiani mama yake yake aliyekubali mkasa huo kufanyika.

Walimwambia wakati huo anatendewa, kwamba kila wanachofanya ni kwa manufaa yake, bila ya kujua athari za kitendo hicho katika maisha yake ya baadaye .

Nchini Cameroon ambako utamaduni huo umekithiri, serikali na mashirika mbalimbali ya haki za binadamu yako yanapambana na uovu kuzuia mateso kwa maelfu ya wasichana.

Athari za kitendo hicho kwa binti huyo wa Afrika Magharibi, sasa imeshakuwa athari endelevu kea binti huyo.

### UKEKETAJI

Suala la ukeketaji wanawake nalo ni sehemu ya mila ambazo zinazopingwa sana katika sehemumbali duniani ikiwamo Afrika na kuna mataifa kama Tanzania, ambako wamefaulu kuiharamisha kisheria, huku harakati za kukomesha utamaduni ikiendelea ndani ya jamii.

Ukeketaji hufanyika kwa njia mbalimbali za siri kuligana na mwenendo wa jamii, mila na umbile la anayetendewa.

***Kwa mujibu wa taarifa ya BBC.***

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Namna halisi Kiswahili kinasuasua kutokana na kukinzana hoja tata




Sehemu ya maudhui ya tamasha linaloendana na kuadhimisha ustawi wa lugha ya Kiswahili. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

KUNA sura moja lugha ya Kiswahili, kwamba kwa kiasi kikubwa imekuwa kwa kasi. Pia katika sura ya pili kuna pengo la baadhi ya maeneo yenye hali ya kusuasua, kuwapo mianya ya misamiati.

Hadi sasa mtazamo ulioko ni wa kuwapo mpangilio sahihi wa kukua lugha ya Kiswahili, hali inavyoendana na kuwapo mvuto wa matumizi ya kawaida ya lugha hiyo.

Kimantiki, kuna mwelekeo unaopiganiwa na wadau wakuu wa lugha hiyo ya taifa, pale panapoonekana kuwapo ukakasi wa msamiati au penye upungufu wa msamiati, kutokana na sababu kama vile kuzaliwa maneno mapya.

Nchini kukiwa ndio mzizi mkuu kimataifa wa mawasiliano ya Kiswahili, kunatajwa pia lugha za wageni walioshi nchini wana mchango ndani ya lugha hiyo ya taifa, iwe katika mazingira yasiyo rasmi na hata huenda rasmi.

Kuna mwingiliano wa mawasiliano ya Kiswahili utokanao na Kiingereza, hasa pale unapotokea mwanya katika misamiati ya Kiswahili. Hata hivyo, wataalamu wa Kiswahili wanasita kupatiwa mbadala wa moja kwa moja.

Ni mantiki inayoangukia mtazamo wa kwamba ni dhamira ya kifalsafa, pia kisaikolojia kwamba Kiswahili kuwa ni utaifa wa lugha, yaani wazungumzaji

> "Ujumla wa yote hayo unatoa hoja ni namna gani ulivyo ukweli na fusra ya msamiati mpya ya Kiswahili ama inaambulia au inaweza kuvumbuliwa.




Kiswahili wajitahidi kukiongea kilivyo ili kisiingiliwe na lugha za kigeni.

Pia panapoonekana upungufu wa kueleza dhana hiyo au ile ya akilini, basi msaada unapaswa kupatikana kuunda neno mbadala, ikiwamo katika namna ijulikanayo kimsamiati kama 'kutohoa.'

Ni wazo linaloingia katika kundi ambalo mshairi na mwandishi maarufu wa riwaya, Marehemu Shaaban Robert alichokiita 'kufikirika' au 'kusadikika,' kwani akiitaja kuwa ni 'taswira pendekezwa' na siyo sura halisi ya kilichopo. Jamii ya Tanzania hadi sasa ni Taifa linalozungumza Kiswahili, pia Kiingereza kwa mahitaji mengi zaidi ya kitaaluma, ndio imetawala.

Wanaosimamia wengi wamejikita katika utetezi na ufuatiliaji wa hitaji hilo 'fikirika' au 'sadikika' na siyo hitaji halisi la watumiaji.

Kila mtu anakopita anakuta maelezo hasa ya kibiashara yanavyounganishwa na maelezo ya Kiingereza, kuainisha ni bidhaa gani inapendekezwa kwa mlaji mtazamiwa, avutiwe na bidhaa inayozungumziwa na kuiagiza au kutumia.

Msingi wake ni kwamba, hali ya kutumia lugha inayoonekana haijakaa sawa kwa wasimamizi ambao wangependelea maelezo hayo 'yawasilishwe' kikamilifu. Kwa ujumla, kuna aina ya walakini namna lugha inavyotumika.

Mathalani, Rais Samia Suluhu Hassan, alipozungumzia mifumo ya ukusanyaji mapato serikalini hivi karibuni , aliwasilisha hoja yake akitumia msamiati wenye mzizi wa Kiingereza kwamba 'hakuna uniformity' kwa maana ya kukosekana mfanano au kuwapo hali ya mianya na akaagiza kurekebishwa kwa hali hiyo, kuzuia upotevu, akitumia tena msamiati 'ku-harmonise.'

Kimsingi, hapo ndiko kwenye mzizi wa msingi wa kukua Kiswahili kutumika kama nyenzo ya kueneza ufahamu wa bidhaa au mifumo ya kitaaluma aina tofauti na ndivyo inavyotakiwa itumike, ili kusiwapo kizuizi cha kuelewa.

Mahitaji ya jamii kitaaluma na kibiashara kwa ujumla, pia ni pale inapogusa bidhaa zisizo za kawaida sokoni (kwa jamii ya jadi), milango ya lugha za kigeni inafunguliwa angalau kidogo, kwani baadhi ya wateja wanaopita kuangalia huduma au bidhaa zinazotolewa.

Huwa kuna wakati wateja wanaongea lugha za kigeni pale wanapokutana na ama huduma au bidhaa zilizoko ni za kigeni na halina msamiati mbadala, hivyo msamiati huo wa kigeni wanaoendelea nao.

Katika mtazamo kama huo, ndio inamfanya mathalan kinyozi hata angefika darasa la saba tu, bado anajua maana ya lugha zitokanaso na Kiingereza, kikiitwa 'ku-crop' ni nini, vivyo hivyo kuweka 'wave.'

Kuna msemo wa Kiingereza ambao mara nyingine mtu anaingia katika dhana za baadhi ya wakereketwa wa lugha ya taifa, yaani 'reinventing the wheel,' yaani kuunda gurudumu upya.

Ujumla wa yote hayo unatoa hoja ni namna gani ulivyo ukweli na fusra ya msamiati mpya ya Kiswahili ama inaambulia au inaweza kuvumbuliwa.

Hapo ndipo mjadala unachukua nafasi yake, kwa haja ya baadhi ya misamiati iliyotoholewa ikahalalishwa, mtazamo ukaangukia katika namna ya kupata uhalali wa misamiati ya kihasibu kama vile 'uniformity'(mfanano), kwa vile imeshazoeleka.

Kwa nini hivyo? Hapo kunajibiwa kwamba kupitia ukweli wa msamiati ya Kiingereza ambayo imesheheni lugha Kilatini, kukiwapo mfanano wake lugha ya Kiswahili, ikiwa na mzizi wa Kiarabu.

Ujumla wake ni kupatikana kile kinachoitwa katika fani ya elimu jamii kwamba 'long waves,' yaani ikimaanisha; mikondo mirefu ya kihistoria katika namna watu wanavyofikiri au kujituma kiitikadi.

Kuna ugumu kama itakumbatiwa Kiarabu pekee kwa sababu za kihsitoria ya Kiswahili na kutokuwapo wepesi kutoa nafasi kwa lugha nyinginezo kuingia ndani ya Kiswahili, mathalani Kiingereza. Inaishia kuzaa mtihani mkubwa.

Mara nyingi kuna utamaduni wa muda mrefu kutoka kwa watetezi wa lugha wanaoangukia katika kundi la watu wa Pwani waliounganika kimkakati katika kukuza lugha hiyo na wasomi, wengi wanatoka Bara.





# Wanakijiji wanufaika ajira za muda TASAF

Na Renatha Msungu, MPWAPWA

WAKAZI wa Kijiji cha Ipwaga na Kidenge vilivyopo wilayani Mpwapwa, wamenufaika na ajira za muda kutoka Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) za ujenzi wa bwawa la maji kwa ajili ya matumizi ya kunywesha mifugo na kilimo cha umwagiliaji.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mwenyekiti wa Kijiji cha Pwaga, Dickson Nzugu, alisema ujenzi wa bwawa hilo umesaidia ajira za muda kwa wakazi wasiopungua 1,500 ambao walilipwa fedha kutokana na ujenzi wa bwawa hilo ambalo sasa wanalitumia kwa ajili ya kunywesha mifugo pamoja na kuendesha kilimo cha umwagiliaji.

"Hapa kijijini kuna takribani wakazi 13,000 ambao awali kabla ya ujenzi wa bwawa tulikuwa tunatembea umbali wa kilomita zaidi ya saba kwenda kunyeshwa mifugo, lakini pia kutafuta maji kwa ajili ya matumizi mengine,"alisema.

Aidha, alisema kukamilika kwa bwawa hilo kumewaondolea adha hiyo.

"Tunaishukuru sana TASAF, imekuwa ikibuni miradi ya kufanya kwa ushirikiano na walengwa ambayo inawasaidia kuwainua kiuchumi wanakijiji,"alisema Mwenyekiti huyo.

Alisema hivi sasa wakazi wa eneo hilo wanaendelea na ujasiriamali kupitia huduma ya maji yatokanayo na bwawa hilo kuendesha shughuli za kilimo pamoja na kunywesha mifugo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Kijiji cha Kidenge, Manase Mkada, alisema TASAF imewasaidia wakazi wa eneo hilo kwa kutoa fedha ambazo zimetumika kuchimba bwawa ambalo hutoa huduma ya maji kwa wakazi hao na vijiji jirani.

Mkada alisema hatua hiyo imesaidia kuinua uchumi wa wanajamii wanaoishi hapo kwa kuanzisha bustani za mboga na ufugaji ambapo hutumia maji hayo kunywesha mifugo yao.

Naye, Ofisa Malalamiko kutoka Idara ya Mawasiliano TASAF, Makwinja Yusup, alisema ajira hizo za muda huwa zinalenga kwa walengwa wa mpango huo ili wajiongezee kipato mbali na fedha wanayopata.

"Hii huwasaidia sana walengwa kujiongezea kipato kutokana na ajira hizo za muda ambazo wanafanya katika mradi husika," alisema Makwinja.

Alibainisha wamekuwa wakihimiza walengwa katika maeneo mbalimbali kuchagua mradi ambao utawapa manufaa wanakijiji kwa ujumla.

# Sababu kesi za ukatili kijinsia kuishia mitaani

Na Renatha Msungu, CHAMWINO

IMEELEZWA kuwa umaskini katika Wilaya ya Chamwino ni miongoni mwa sababu kesi za katili wa kijinsia kuishia mitaani badala ya kufikishwa kwenye vyombo vya dola.

Suala hilo liliibuka mwishoni mwa wiki katika mkutano wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ulioandaliwa na Shirika lisilo la kiserikali la Women Wake Up (Wowap) kwa kushirikisha kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto ngazi za kata na vijiji.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Mtendaji wa Kijiji cha Mwegamile, Nassoro Shaban, alisema jamii imekuwa ikiibua matukio, lakini mashauri hayo yamekuwa hayafiki mwisho mzuri.

Alisema mashauri hayo yanapofika katika ofisi za mtendaji wa kijiji au kata na watendaji wanapochukua hatua ya kufikisha kesi hizo mahakamani huchukuliwa kama ni watu wanaoingilia mambo yasiyowahusu.

"Tunajitahidi tuwezavyo kuhakikisha haki inatendeka ikiwamo kwenda kutoa ushahidi mahakamani, unang'ang'ania mtu, lakini mwisho wa siku anaachiwa huru na mahakama," alisema Shaban.

Alisema wazazi wamekuwa na tabia ya kumalizana wao kwa wao ili kupoteza ushahidi hasa pale tukio linapofanywa na ndugu wa karibu au jirani na kupewa fedha au mifugo ili kesi isiendelee.

"Kwenye kijiji changu mwanafunzi alipata ujauzito ,mama wa binti anauza pombe za kienyeji kwa hivyo alikuwa hamfuatilii binti yake, kijana aliyempa mwanafunzi ujauzito akakamatwa kesi ikaenda mahakamani ikasikilizwa kijana akashinda kesho yuko mtaani," alisema.

Kwa upande wake, Ofisa Ustawi wa jamii wilayani humo, Lucas Kaombwe, alisema mpango huo ulianzishwa mwaka 2017 na unatakiwa kufanyiwa tathmini ifikapo 2022.

Alisema kila halmashauri ina mpango wa kutokomeza ukatili wa kijinsia na kwamba kamati ya ulinzi wa wanawake na watoto katika ngazi ya Halmashauri ndio itaratibu shughuli zinazohusiana na mpango na kuboresha utoaji wa huduma kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi. Hata hivyo, alisema kikwazo kilichopo ni wasichana wanaopata ujauzito wamekuwa wakisita kuwataja wahusika.

Naye, Mratibu wa mafunzo hayo, Nasra Suleiman kutoka Wowap, alisema mafunzo hayo yanalenga kuziwezesha kamati, kuzijengea uwezo na maarifa katika ngazi ya kata na vijiji.

"Tunafanya kazi ya utetezi wa haki za mtoto, kimsingi kamati zinaundwa na serikali katika mpango wa kutekeleza ukatili kwa watoto kuhakikisha unaondoshwa," alisema.



Wabebataka wa Soko la Sabasaba Jiji la Dodoma, wakimwanga taka kwenye makontena yaliyowekwa na Halmashauri ya Jiji jana, kwa ajili ya shughuli hiyo kwa wafanyabiashara na watumiaji wa soko hilo. PICHA: PETER MKWAVILA

# 'W'biashara pangeni bidhaa maeneo safi'

Na Peter Mkwavila, DODOMA

OFISA Masoko wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, James Yuna, amewataka wafanyabiashara kuhakikisha wanapanga bidhaa zao kwenye maeneo safi ili kulinda afya za walaji.

Yuna aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi habari baada ya uchaguzi wa viongozi wa wafanyabiashara wa soko la sabasaba, jijini humo.

Ofisa huyo alisema kuwa Dodoma ni makao makuu ya nchi hivyo kwa wafanyabiashara wakahakikisha maeneo wanayofanyia biashara yanazingatia afya za walaji na kukidhi soko la ushindani wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi.

"Rai yangu hapa ninawaomba wafanyabiashara kufanya shughuli zao katika mazingira yenye ubora na kuzingatia kanuni za kiafya, hii itawafanya kuwavutia wateja na walaji wa bidhaa zao na kuingia kwenye ushindani wa biashara,"alisema.

Aliwasisitiza kuheshimu na kutii kanuni na taratibu katika ufanyaji biashara na kujiepusha kuvamia maeneo yasiyo rafiki ambayo hayaruhusiwi.

Alisema pamoja na uhuru walionao wa kufanya biashara, wafanyabiashara wanawajibu wa kushirikiana na Jiji katika kuhakikisha maeneo yasiyo rasmi wanayaepuka na kufuata maelekezo yanayotolewa.

Kuhusu viongozi wa soko la Sabasaba, ofisa huyo aliwaomba kuhakikisha wanashirikiana na Jiji ili kuhakikisha wafanyabiashara wanafuata kanuni na maelekezo yanayotolewa.





# Maagizo ya Samia yawakuna w'biashara

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

BAADHI ya wafanyabiashara mkoani Mbeya, wamesema maagizo yaliyotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa maofisa wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuacha kutumia nguvu kukusanya kodi yameleta matumaini mapya kwao.

Aprili Mosi, mwaka huu wakati akiwaapisha mawaziri, Rais Samia alipiga marufuku matumizi ya nguvu kwenye ukusanyaji wa kodi akidai kuwa utaratibu huo unasababisha biashara nyingi kufungwa.

Aidha, alimwagiza Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kutanua wigo wa walipakodi kwa kuacha kutumia nguvu na badala yake akawataka kutumia akili.Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, wafanyabiashara hao walisema maagizo hayo ya rais endapo yatatekelezwa kwa vitendo, Tanzania itakuwa moja ya mataifa yenye wafanyabiashara wengi wakubwa.

Elius Ngisi alisema utaratibu uliokuwapo uliwafanya wafanyabiashara wawaone maofisa wa TRA kama maadui wao hasa walipokuwa wanakwenda kudai kodi.

Alisema wakati mwingine maofisa hao walikuwa wanalazimisha kufunga biashara zao na kuwataka wafanyabiashara hao wakalipe kwanza kodi ndipo wafunguliwe biashara zao.

"Rais ameonyesha kuwa ana lengo la kutusaidia kukua kiuchumi ili na serikali ikusanye kodi kwa ajili ya uendelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, tulikuwa tunakimbizana na maofisa wa TRA utadhani sisi ni wahalifu," alisema Ngisi.

Naye Mariam Mwaikambo, mfanyabiashara katika Soko la Sido, alisema kuna baadhi ya wafanyabiashara walikuwa wanahamisha biashara zao na kuzipeleka katika mataifa jirani ili kuzinusuru zisife.

Alisema waliokuwa wanaendelea na biashara katika kipindi kilichopita ni wale wavumilivu, lakini ambao sio wavumilivu walikuwa wanalazimika kufunga biashara zao ili wakafanye shughuli zingine, lakini kauli ya rais imeanza kufufua matumaini yao.

Mariam alisema serikali inatakiwa kuwa mlezi wa wafanyabiashara badala ya kuwa adui wao na kwamba maofisa wa TRA wanatakiwa kutumia zaidi mbinu ya kuwaelimisha wafanyabiashara kuliko kutumia nguvu kama alivyoagiza Rais.

"Majirani zetu Zambia wanapitisha mizigo yao nchini kwetu kupeleka kwao, lakini mizigo mingi wanauza kwa bei nafuu kuliko sisi wenye bandari, ndio maana baadhi ya wafanyabiashara huwa wanaenda kununua vitu Zambia na Malawi na kuviingiza nchini kupitia njia za panya," alisema Mariam.

Aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu', aliandika kwenye ukurasa wake wa 'Tweeter' kuwa kitendo cha kuwaita Watanzania kuwa ni wanyonge ni kuwadhoofisha.

Juzi wakati wa maadhimisho ya Pasaka, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisisitiza maofisa wa TRA maagizo yaliyotolewa na Rais Samia kuhusu utaratibu wa ukusanyaji wa mapato, huku akisisitiza kuwa Wizara ya Fedha imepewa malengo ya kukusanya Sh. trilioni mbili kwa mwezi.



Baadhi ya waumini wa Kanisa la Moravian Tanzania Ushirika wa Iwambi jijini Mbeya, wakifuatilia mahubiri ya Sikukuu ya Pasaka juzi, yaliyokuwa yanaendeshwa na Mchungaji wa Kanisa hilo, Antony Ntove. PICHA: NA NEBART MSOKWA.

# Wakulima waitwa kupima afya ya udongo

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya imewataka wakulima kujitokeza kupima afya ya udogo wa mashamba yao ili kuepusha hasara wanayoipata kutokana na tindikali nyingi inayoathiri uzalishaji wa mazao.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, aliyasema hayo wakati akizungumza na wakulima mkoani Mbeya kuhusu madhara ya kuzidi kwa tindikali kwenye udongo katika uzalishaji wa mazao hasa ya chakula.

Alisema utafiti uliofanywa na Kituo hicho umebaini kuwa mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini inakabiliwa na tatizo la wingi wa tindikali kwenye udongo na kwamba endapo hatua za haraka hazitachukuliwa taifa linaweza kukumbwa na uhaba wa chakula kutokana na wakulima kutozalisha mazao ipasavyo.

"Tumefanya utafiti na kubaini kuwa hili tatizo la wingi wa tindikali kwenye udongo lipo katika mikoa yote ya Nyanda za Juu Kusini, lakini pia tumeshagundua njia ya kudhibiti tatizo hilo, hivyo ni suala la wakulima kujitokeza kupima afya ya udongo wa mashamba yao na sisi tutamshauri hatua za kuchukua," alisema Bucheyeki.

Alisema kuwa tatizo la wingi wa tindikali kwenye udongo linasababisha mimea ya mazao kutostawi vizuri na hivyo kupungua kwa uwezo wake wa kutoa mazao hali ambayo inaweza kuwasababishia wakulima hasara kubwa na hata taifa kukubwa na uhaba wa chakula.

Mtafiti wa Udongo kutoka TARI Kituo cha Uyole, Fredrick Mlowe, alisema kuwa utafiti uliofanywa na kituo hicho unaonyesha kuwa shamba lenye ukubwa ekari moja likiwa halijatibiwa tiba ya udongo kutokana na wingi wa tindikali likilimwa zao la mahindi linao uwezo wa kutoa magunia kati ya saba mpaka nane, lakini likitibiwa linaweza kuongeza mavuno mpaka kufikia magunia 35.

"Tiba ya udongo ikifanyika kudhibiti wingi wa tindikali kwenye mashamba, ni ukombozi kwa wakulima kwa sababu kwa sasa wanatumia gharama kubwa ya kulima na kutunza mimea yao, lakini wanapata mavuno kidogo sana, lakini wakiyatibu mashamba yao kwa kutumia gharama hizo hizo wanaweza kuongeza uzalishaji mara dufu na hivyo kupata kipato kikubwa," alisema Mlowe.

Johnson Mtama, Mtafiti wa Udongo kutoka TARI kituo cha Uyole, alisema tiba ya udongo wenye tindikali nyingi imebainika kuwa ni kuongeza madini aina ya chokaa mashambani.

Alisema kiasi cha chokaa kinachohitajika kinategemeana na vipimo vya maabara vya udongo katika eneo husika hivyo akawataka wakulima kuleta sampo za udongo wa mashamba yao ili upimwe kabla ya kupewa ushauri wa kutibu mashamba yao kwa kutumia chokaa.

Alisema TARI Uyole inavyo vifaa vya kisasa vya kupima afya ya udongo na kutoa majibu kwa haraka hivyo wakulima wajitokeze kwa wingi ili kumaliza tatizo la wingi wa tindikali kwenye mashamba yao.

## Wakulima wa vitunguu wataka soko la uhakika

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

WAKULIMA wa vitunguu katika Bonde la Utengule katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali kuwasaidia kutafuta soko la uhakika nje ya nchi ili wanufaike na zao hilo kwa kuinua uchumi wao.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakulima hao walisema soko la ndani haliwanufaishi kutokana na zao hilo kuuzwa kwa bei ya chini kuliko gharama za uzalishaji.

Enock Mwasile, alisema bei ya zao hilo kwa sasa haieleweki kwa maelezo kuwa kuna kipindi walikuwa wanauza gunia moja kati ya Sh. 100,000 na 150,000 hali ambayo ilisababisha wakulima wengi kuhamasika kulima.

Alisema kwa sasa bei imeshuka mpaka Sh. 40,000 hali ambayo alisema inakatisha tamaa na baadhi wameanza kuacha kulilima na kuamua kulima mazao mengine.

"Tunalima hili zao tukitegemea soko la ndani na hatujui ni wapi kwingine tunaweza kuuza, tunaiomba serikali itusaidie tupate soko la nje ambalo litakuwa na faida zaidi, ukilima ekari moja unaweza ukatumia Sh. 450,000 mpaka 500,000 kuhudumia lakini unauza unapata 600,000 baada ya miezi mitatu mpaka minne," alisema Mwasile.

Naye Malezi Njila, alisema kati ya mwezi Desemba na Februali soko la zao hilo huwa linapanda mpaka Sh.100,000 kwa gunia lakini utunzaji wa zao hilo ni mgumu kutokana na kuoza endapo litagusana na maji.Alisema kuna kipindi alivuna gunia 20 akazihifadhi ndani kumbe nyumba inavuja na hivyo alipotaka kuuza aligundua kwamba asilimia kubwa ya vitunguu hivyo vilikuwa vimeoza na vingine vimeota hali ambayo iliharibu soko.

Alisema yeye kwa sasa analima zao hilo kwa sababu hana uzoefu wa kulima mazao mengine na kwamba wenzake walishaacha na kuingia kwenye kilimo cha alizeti ambacho hata yeye anakusudia kuanza mwaka huu.

"Huwa tunasikia wenzetu wa Singida wanalima na kupata soko zuri, sasa hatuelewe wenzetu wanafanikiwa vipi, ni vizuri serikali ikatuunganisha na sisi kwenye soko la wenzetu," alisema Njila.Vitunguu ni miongoni mwa mazao ya bustani ambayo wakulima wamekuwa wakishauriwa kuyazalisha katika Mkoa wa Mbeya, lakini wakulima wanadai halina soko la uhakika.



## Jamii yatakiwa kuchangamkia mafunzo ya ndoa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

JAMII imetakiwa kuendelea kujitokeza kwa wingi katika mafunzo ya ndoa ili kupata amani na utulivu wa moyo katika maisha ya ndoa na vizazi vilivyo bora vyenye kufuata misingi na maadili mema.

Hayo aliyasema Mufti wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, wakati wa kufunga mafunzo ya ndoa awamu ya tisa katikaUkumbi wa Masjid Jaamiiu Zinjibar Mazizini Zanzibar.

Alisema kuna umuhimu mkubwa wa kila mtu kupata mafunzo ya ndoa na yanapelekea kujengeka kwa familia zilizo imara na malezi bora kwa watoto.

Alisema ndoa huwalinda watu na machafu ikiwamo zinaa ambayo husababisha maradhi mbalimbali ya kuambukiza, hivyo ni vyema wanandoa kuzitunza ndoa zao ili kuepukana na machafu hayo.

"Ukiwa na ndoa yenye utulivu, mawada na mahaba utaepukana na uzinifu, ukiacha zinaa umejilinda na kaswende, gono hata Ukimwi tujitahidini kuzitunza ndoa zetu," alisema Mufti.

Sheikhe Kabi aliwasisitiza washiriki wa mafunzo hayo kuyafanyia kazi na kuwa walimu kwa wale ambao hawajapa nafasi hiyo kutokana na sababu mbalimbali ili kuleta mabadiko chanya katika ndoa na jamii kwa ujumla.

Akitoa maelezo ya mafunzo hayo Mkuu wa kitengo cha Fatwa na utatuzi wa migogoro, Ali Muombwa Hasan, alisema jumla ya wanafunzi 1,293 wamehitimu mafunzo hayo kutoka mwaka 2018 hadi 2021 kwa Zanzibar nzima.

Washiriki wa mafunzo hayo katika risala yao walisema elimu waliyoipata wataitumia vyema kwa lengo la kupunguza au kuisha kabisa kwa talaka kwa wale waliomo na wanaotaka kuingia kwenye ndoa, kutatua migogoro katika familia pamoja na kuwa na nidhamu, subira na ujasiri katika kujenga ndoa zenye mahaba na mawada ili ziendee kudumu.

Harith Auni Muhammed akisoma risala hiyo, aliishauri Ofisi ya Mufti kuingizwa somo la ndoa na talaka katika mitaala ya masomo kwa wanafunzi wa kidato cha tatu hadi vyuo vikuu.

# Makamu wa Kwanza wa Rais ashauriwa mazingira

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KAMATI ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi imemuomba Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kusimamia maslahi ya Zanzibar kwenye mazingira kutokana na miradi ya kimataifa inayohusu na suala hilo kuingizwa kwenye mambo ya Muungano.

Akizungumza kwenye Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliyopo Migombani Mjini Unguja, Mwenyekiti wa kamati hiyo, Hassan Khamis Hafidh, alisema kwamba Zanzibar, ambayo ni nchi ya visiwa, inaathirika sana na mabadiliko ya tabianchi, lakini imekuwa haifaidiki sana na miradi ya kimataifa na inapofika inakuwa si kwa wakati.

"Makamu, tunakuomba sana suala hili mlione na mulizungumze, ikibidi hata kama ni mgao unaotolewa kuhusu mazingira, basi utufike na utufike kwa wakati, kwani hata huku Zanzibar wapo watu wenye weledi katika suala la kimazingira, lakini kama kuna changamoto, ndio eneo sahihi kwetu kujifunza," alisema mwenyekiti huyo.

Hassan alielezea jinsi ambavyo kuingizwa suala la mazingira katika Muungano kunavyoikosesha Zanzibar fursa, misaada na miradi ya moja kwa moja, kwa kuwa shughuli zote zinazohusiana na suala hilo humalizika Tanzania Bara, na inapotokea kuletwa Zanzibar huwa ni kwa hatua za utekelezwaji tu.

Aidha alisema Idara ya Mazingira, ambayo iko chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ni miongoni mwa idara muhimu sana kwa taifa na uwepo wa mazingira salama maisha ya wananchi nayo huwa salama.

"Mheshimiwa Makamu, tunakupongeza sana kwa kuona idara hii ya mazingira ipo kwako, maana tunaamini wewe na waziri wako, ni watu sahihi sana katika eneo hili, na bila shaka tunategemea mabadiliko makubwa," alisema mwenyekiti huyo.

Kwa upande wake, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud, alisema ni kweli kuwa suala la mazingira ni sehemu ya Muungano kwa muda mrefu sana, lakini ni vyema kuzungumzwa na kusawazishwa ili kila upande wa Muungano unufaike.

"Kwa sasa inabidi tumtumie waziri wetu, Mheshimiwa Saada Mkuya, ili kututafutia wafadhili binafsi kutoka maeneo mbalimbali ya dunia ili nasi Zanzibar tuweze kunufaika moja kwa moja na miradi ya mazingira," alisema Makamu huyo wa Rais.



Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, akizungumza kuhusu mafunzo ya ndoa katika hafla ya kufunga mafunzo hayo iliyofanyika Ukumbi wa Masjid Jamiu Zinjibar Mazizini Zanzibar. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Hemed awapa majukumu maofisa elimu

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah, amesema maofisa wa elimu wanapaswa kijipanga vyema katika kuhakikisha ufaulu wa wanafunzi katika shule unaongezeka.

Alisema taifa linahitaji kuwa na wataalamu wa kutosha watakaokuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi kutokana na utaalamu wao utaoambatana na uzalendo, hivyo kuleta mafanikio makubwa.

Aliyasema hayo baada ya kutoridhika na matokeo ya ufaulu katika Wilaya ya Wete Pemba kufutia taarifa ya Serikali ya wilaya hiyo katika Chuo cha Bendjamin Mkapa Mchangamdogo wakati wa ziara zake za kukagua miradi ya maendeleo na kuona changamoto zinazowakabili wananchi wa wilaya zote za Unguja na Pemba.

Alisema zipo sababu zisizokuwa za msingi zinazoendelea kutolewa na baadhi ya wasimamizi wa elimu kwa kisingizio cha mabadiliko ya mitaala, jambo ambalo halikubaliki kwa vile ndani ya mabadiliko hayo unatokea ufaulu kwa wanafunzi kwenye shule hizo.

Hemed alieleza masikitiko yake kuona kwamba pale inapotokea fursa ya ajira hata katika nafasi ya uhudumu hujitokeza waombaji wengi kwa nafasi chache, lakini pale wanapohitajiwa uthibitisho wa vyeti ndipo unapojitokeza ubabaishaji wa vielelezo hivyo vinavyokosa sifa stahiki.

Alisisitiza umuhimu wa kuimarishwa mikakati ndani ya kamati za shule zitakazoshirikiana na viongozi wao wa Serikali za Mkoa, wilaya na jimbo itakayokuwa chachu ya kuzirejeshea sifa za ufaulu shule mbalimbali nchini zilizotoa wataalamu ambao kwa sasa wanaendelea kulitumikia Taifa.

Akiangalia kilimo cha mazao ya viungo katika shamba la Daya Cooperative Society Pemba, Makamu wa Pili wa Rais aliwapongeza wakulima hao kwa umahiri wao wa kuanzisha kilimo cha viungo kilichoonyesha muelekeo wa upatikanaji wa soko na kipato kikubwa.

Aliwapa moyo wakulima hao kwa kuwataka waendelee kuimaisha zaidi kilimo chao cha viungo hasa lile zao la vanila ambalo tayari limeshafikia thamani ya Sh. 750,000 kwa kilo moja.

Alimuagiza Afisa Mdhamini Wizara ya Kilimo Pemba na wataalamu wake kukaa pamoja na wakulima hao, kuangalia changamoto zinazowakabili ikiwemo utaalamu na akautaka uongozi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) kuangalia mazingira ya kutoa mikopo kwa wakulima vijijini.

Kuhusu mtambo wa kukaushia bidhaa za viungo, alisema jumuiya za kiraia zimekuwa na mchango mkubwa katika kuisaidia Serikali kwenye miradi inayowagusa moja kwa moja wananchi hasa wakulima. Wakati huo huo,

Hemed alitembelea Hospitali ya Wilaya Wete kuona utoaji huduma za afya kwa wananchi na kutoridhika na huduma kwa baadhi ya vitengo vya hospitali hiyo vilivyosimamisha kutoa huduma.Hemed alitoa agizo kwa uongozi wa Wizara ya Afya kufanya marekebisho ya haraka kwa chumba cha maalum cha wagonjwa mahututi (ICU), X-ray na cha kuhifadhi maiti ili vitengo hivyo viendelee kutoa huduma kama kawaida.

# Wakazi wajitolea kuboresha kingo mto kuepuka mafuriko

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WAKAZI wa mtaa kwa Omukigusha, Kata Bilele mkoani Kagera, wanaokumbwa na adha ya mafuriko msimu wa mvua, wamejitolea kuboresha kingo za mto Kanoni na kuondoa mchanga ili kuruhusu maji kupita na kuepuka kukumbwa na mafuriko.

Wakizungumza na Nipashe, mmoja wa wakazi hao, Mansuri Omary, alisema wameamua kutumia nguvu zao kuboresha mazingira ya mto huo kwa kushirikiana na viongozi wa serikali ya mtaa kwa lengo la kuepusha madhara yanayowakumba mara kwa mara katika msimu wa mvua.

"Mvua zikinyesha mto unajaa na maji huingia katika makazi yetu na kuharibu mali, kutokana na hilo tumeona tujitolee nguvu zetu kurekebisha kingo za mto, kuondoa mchanga na kujaza udongo kwenye viroba ili kuzuia mmomonyoko wa udongo, lengo kikiwa ni kupunguza hofu kwa wananchi," alisema Mansuri.

Wananchi kwa kushirikiana na viongozi wao waliunda kamati ya kushughulikia changamoto hiyo ambayo pamoja na mambo mengine husaidia kutoa taarifa kwenda kujitolea kuboresha mazingira ya mto huo.

Katibu wa kamati hiyo, Mwinyi Mohamed, alisema mafuriko yaliyotokea siku za nyuma yalikuwa ya hatari, lakini baada ya kuundwa kwa kamati hiyo ambayo huhamasisha wananchi na kuelimishana jinsi ya kukabiliana na adha za mto huo, wamepunguza madhara kwa kiwango kikubwa.

"Wananchi sasa nao wanajitoa sana kuboresha mazingira, leo takriban wananchi 200 wamefika kujitolea, tunaomba serikali yetu itusaidie kupata ufumbuzi wa kudumu katika maeneo yetu ili tuishi salama," alisema Mwinyi.

Naye Mwenyekiti wa mtaa wa Omukigusha, Abdurahakimu Idrisa, alisema kuwa wamefikia uamuzi huo ili kudhibiti maji ya mto huo ambayo yamekuwa yakiingia katika makazi ya watu kila msimu wa mvua na kuharibu mali.

"Mwaka 2020 tulifanya kazi hii tukanusurika na mafuriko, tumeona na mwaka huu tufanye tena maana hapa ni eneo korofi kila mwaka husababisha maafa, tuna imani tutamaliza msimu wa mvua za masika salama," alisema.

Akieleza alivyosaidia wananchi wake kukabiliana na tatizo hilo, Diwani wa Kata Bilele, Tawfiq Salum, alisema kwa kushirikiana na Mbunge wa Jimbo la Bukoba Mjini, Stephen Byabato, tatizo hilo limefikishwa katika manispaa hiyo ili kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu.

"Katika bajeti ya mwaka 2021/2022 tumepeleka mapendekezo ya Sh. milioni 500 serikali kuu, ambazo ni kwa ajili ya kutengeneza kingo za mto Kanoni pekee, hili tatizo litakwisha wananchi wanapaswa kuendelea kuwa wavumilivu," alisema Tawfiq.

Hivi karibuni akitoa tahadhari baada ya kuanza kwa mvua za masika, Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Deodatus Kinawiro, aliwataka wananchi wa maeneo yenye hatari ya kukumbwa na mafuriko yakiwamo ya Omukigusha, Buyekera na Nyamkazi kuchukua tahadhari ikiwamo kuhama kwa muda katika maeneo hayo ili kupunguza madhara.




Mafundi wakiendelea na ujenzi wa barabara ya mabasi ya mwendo kasi (BRT phese 2) katika eneo la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMAMNE JUMA**

## Wakulima wadai kupata hasara

**Na Thobias Mwanakatwe,** KISARAWE

WAKULIMA wanane wa vijiji vitatu vilivyopo Kata ya Mkumbulu, wilayani Kisarawe, mkoani Pwani, wamepata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 460 kutokana na ekari 170 walizokuwa wamepanda mpunga kuharibika baada ya kufukuzwa katika eneo walilokuwa wakilima.

Wakulima hao wa vijiji vya Kitonga Chole, Panga la Mwingereza na Mtunani walifukuzwa na askari wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Tanzania (TAWA) na kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa madai walikuwa wakilima ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere, zamani ikiitwa Selous.

Katibu wa Kikundi cha wakulima walioathirika baada ya kukamatwa na askari wa TAWA, Gasper Matovu, aliwataja wakulima waliokamatwa ni Mosty Mwasenga, Matata Mlete, Rajabu Jonas, Mashaka Kidaha, Idd Mambosasa, Daudi Kidaha, Mabula Kidaha na Abdallah Said.

Matovu akizungumza katika mkutano wa viongozi wa vijiji hivyo, alisema wakulima hao baada ya kukamatwa walifunguliwa kesi namba 55/2019 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro kwa madai kuwa walikuwa wakilima ndani ya hifadhi.

Hata hivyo, upelelezi wa kesi hiyo ulipofanyika ilibainika kuwa wakulima walikuwa wakilima kwenye eneo halali la kijiji na siyo hifadhi hali iliyomfanya Mwanasheria wa Serikali kuiondoa kesi hiyo Julai 29, 2019 (nyaraka tumeziona).

Mmoja wa wakulima waliokamatwa Mosty Mwasenga, alisema mbali na kukamatwa walinyang'anywa trekta mbili, jembe, mbegu na vifaa vingine vingi. Alisema baada ya kesi hiyo kuondolewa mahakamani vifaa hivyo vilirejeshwa na kukabidhiwa kwa wakulima Februari 11, mwaka huu ikiwa ni miaka miwili tangu vilipokamatwa, huku vingine vikiwa vimeharibika kutokana na kukaa muda mrefu bila kutumika.

"Kesi ilipofutwa shamba la mpunga ekari 170 zilizokuwa zimepandwa zilikuwa zimeharibika na kusababisha hasara ya zaidi ya Sh. milioni 390 na milioni 70 ilitokana na vifaa walivyokamatwa navyo kuharibika," alisema.

# Wanakijiji wilayani Nyasa wapata maji ya bomba

**Na Gideon Mwakanosa,** NYASA

SERIKALI imewatua ndoo kichwani wananchi wa Kijiji cha Chimate, Wilaya ya Nyasa, mkoani Ruvuma, baada ya kutekeleza mradi wa maji uliogharimu Sh. milioni 390.

Akisoma taarifa ya mradi huo, Meneja wa RUWASA Wilaya ya Nyasa, Mhandisi Jeremia Maduhu alisema mradi huo ambao umekamilika kwa zaidi ya asilimia 85 unatekelezwa kupitia force account.

Alisema mradi huo utakapokamilika, unatarajia kuhudumia wananchi wa Kijiji cha Chimate wapatao 2,798, na kwamba maandalizi ya mradi huo yalianza Juni 2020 ambapo kazi rasmi ya ujenzi wa mradi ilianza Julai Mosi, 2020.

"Kazi zilizopangwa kutekelezwa kwenye mradi huu ni ujenzi wa chanzo kipya cha maji, ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa meta 75,000, ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 15, ujenzi wa mtandao wa bomba wenye urefu wa kilometa 15," alisema Maduhu.

Alisema mradi huo hadi sasa umetumia zaidi ya Sh. milioni 356, na kwamba unatarajia kukamilika kwa asilimia 100 mwezi huu.

Alizitaja kazi zilizokamilika kwa asilimia 100 ni ujenzi wa chanzo kipya cha maji, tanki la kuhifadhia maji na ujenzi wa vituo 18 vya kuchotea maji.

Akizungumza baada ya kuweka jiwe la msingi kwenye mradi huo, Mkuu wa Wilaya ya Nyasa, Isabela Chilumba, alisema ni jambo la kufurahisha kwamba ameweka jiwe la msingi kwenye mradi huo wakati vituo 10 kati 18 vinatoa maji na kuwataka wananchi hao kutunza mradi huo.

Chilumba aliwapongeza RUWASA kwa kusimamia kikamilifu mradi huo kuanzia ujenzi hadi kukamilika hali ambayo sasa itawawezesha wananchi wa Chimate kupata maji safi na salama.

Meneja wa RUWASA Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Rebman Ganshonga, alitoa rai kwa wananchi wa kijiji cha Chimate kuhakikisha kuwa wanasimamia, kutunza na kukilinda chanzo cha maji ili mradi huo uwe endelevu.

## HABARI KIMATAIFA

# Jeshi Msumbiji ladai kuua waasi

**Palma,** MSUMBIJI

VIKOSI vya Msumbiji katika operesheni ya kujaribu kuudhibiti mji wa Kaskazini Mashariki mwa Palma, vimedai kuwaua waasi.

"Bado peresheni haijamalizika, lakini idadi kubwa ya magaidi wameuawa kwa katika operesni hiyo," Kamanda wa Operesheni Palma, Chongo Vidigal, aliwaambia waandishi wa habari.

Siku 11 zilizopita, makundi yenye silaha yalishambulia mji wa bandari wa kimkakati katika uvamizi ulioandaliwa kwa uangalifu, uliozinduliwa kilomita chache kutoka eneo kunakoendeshwa mradi wa gesi unasimamiwa na kampuni ya Kifaransa ya TOTAL.

Maelfu ya wakazi wa mji wa Pwani wa Palma nchini Msumbiji bado wanayakimbia makazi wakihofia usalama wao, baada ya magaidi kuvamia mji huo wiki mbili zilizopita na kusababisha maafa.

Wakazi hao wa Palma walikimbilia mjini Pemba na wengi wao walisema wanaogopa kurejea tena nyumbani. **RFI**



Wakazi wa Kisiwa cha Dili, wakishuhudia athari za mafuriko katika eneo la Mashariki mwa nchi ya Timor na Indonesia mwishoni mwa wiki, kukumbwa na mvua kubwa na kusababisha maporomoko ya udongo, maji kufurika na miundombinu kuharibika, huku watu 101 wakiripotiwa kufa hadi jana. **PICHA: AP**

## EU yataka wapiganaji kuondoka Libya

**Tripoli,** LIBYA

UMOJA wa Ulaya (EU), umetoa wito wa kuondoka kwa wanajeshi wa kigeni na wapiganaji mamluki nchini Libya, ukisema hilo ni sharti muhimu kuelekea kurejea kwa uthabiti wa taifa hilo lililoharibiwa kwa vita.

Akizungumza na waandishi habari kwenye mji mkuu wa Libya, Tripoli, Rais wa Baraza Kuu la Umoja, Charles Michel aliye ziarani nchini humo, alisema ni lazima wapiganaji kutoka nje waondoke na kutoa nafasi kwa Libya kujiimarisha upya.

Michel pia alitoa wito kwa pande hasimu za siasa nchini Libya, kutumia nafasi iliyopatikana ya kuundwa kwa serikali ya mpito kujenga taifa thabiti na lililostawi akiitaja hatua ya kupatikana serikali hiyo kuwa jambo la kihistoria.

Ripoti ya hivi karibuni kabisa iliyotolewa na wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN), ilizituhumu serikali za kigeni kwa kuigeuza Libya kuwa uwanja wa mapambano.

Wataaalamu hao walizitaja Uturuki na Qatar kuwa waungaji mkono wakubwa wa vikosi vya wapiganaji wa serikali inayotambuliwa kimataifa iliyokuwa na makao yake mjini Tripoli. **DW**

## Vifo mafuriko Indonesia vyafikia 100

**Jakarta,** INDONESIA

VIFO vilivyotokana na mafuriko pamoja na maporomoko ya udongo, vimefikia 101 kutoka idadi ya awali iliyokuwa 44.

Mwishoni mwa wiki katika nchi za Indonesia na Timor Mashariki, mvua kubwa zilizonyesha katika nchi hizo zilisababisha maafa huku maji ya mafuriko yakivunja kingo za mabwawa na kusomba maelfu ya makazi ya watu.

Maeneo yaliyoathirika zaidi ni kuanzia kisiwa cha Flores, Mashariki mwa Indonesia hadi nchi jirani ya Timor Mashariki.

Nchini Indonesia pekee, watu 80 walifariki na huku makumi wakiwa hawajulikani walipo. Mamlaka zimetahadharisha kuwa idadi ya vifo inaweza kuongezeka.

"Matope, hali mbaya ya hewa pamoja na kifusi kikubwa kinachoendelea kujikusanya vimekuwa vikwazo vikubwa kwa shughuli za uokozi," Msemaji wa Shirika la Indonesia la kukabiliana na Majanga, Raditya Jati aliwaambia wanahabari.

Takriaban watu 21 pia walifariki katika nchi ya Timor Mashariki, ambayo pia inafahamika kama Timor Leste, maofisa wa nchi hiyo walinukuliwa wakithibitisha.

Waliojeruhiwa katika maeneo ya visiwani waliondolewa na kupelekwa vijiji jirani, pamoja na hospitali na vituo vya afya.

Mafuriko na maporomoko ya udongo hutokea mara kwa mara, nchini Indonesia wakati wa msimu wa masika, ambao kawaida huanzia Novemba hadi Machi. **BBC**

## MwanaMfalme Jordan kukaidi amri ya jeshi

**Amman,** JORDAN

MWANAMFALME, Hamzah al-Hussein wa Jordan, ambaye anaripotiwa kushikiliwa kwenye kifungo cha nyumbani, amesema atakaidi amri ya jeshi, ikimtaka kuwa kimya.

Sauti ya mwanamfalme huyo, iliyotumwa mtandaoni ilisema kwamba, hatakubali kuzuiwa kutoka nje, kutuma ujumbe kwenye ukurasa wa Twitter ama kuwasiliana na watu wengine.

Ndugu huyo wa baba mmoja wa Mfalme Abdullah wa Pili wa Jordan, aliripoti kuzuiliwa tangu jana, huku serikali ikisema imezuwia jaribio la mapinduzi, ingawa haikumtaja Hamzah kuhusika na jaribio hilo.

Mama yake, Hamzah, Malkia Noor, alisema mwanawe na wenzake wengine wanaoshikiliwa ni waathirika wa kile alichokiita fitina ovu.

Mwanamfalme Hamzah ndiye alitakiwa kuwa mrithi wa kiti cha ufalme, kwa mujibu wa wosia wa baba yao, Mfalme Hussein, ingawa baadaye Mfalme Abdullah wa Pili wa Jordan, alimuondoa kwenye nafasi hiyo. **DW**

# MARTIAL NJE YA DIMBA MSIMU MZIMA



**MANCHESTER,** England

ANTHNONY Martial anaweza kukosa kipindi chote cha msimu kilichobaki baada ya kuumia goti, kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amethibitisha.

Mshambuliaji huyo aliumia goti wakati akiichezea Ufaransa dhidi ya Kazakhstan wikiendi iliyopita.

Licha ya kutokuwa katika ubora wake msimu huu, akilinganishwa na alivyokuwa msimu uliopita, Martial bado ni mchezaji muhimu kwenye kikosi cha kocha Solskjaer ambaye anatumia zaidi mfumo wa kushambulia.

Uhodari wa kumiliki mpira sambamba na kasi yake, ni vitu ambavyo Man United itavikosa kwa takribani michezo nane iliyosalia kwenye Ligi Kuu England pamoja na mashindano ya Ligi ya Europa.

Akizungumzia hali ya Martial, kocha wa Man United, Solskjaer alisema, "Kumkosa Martial kwa kipindi chote cha msimu, inakatisha tamaa sana.

"Taarifa kutoka Ufaransa zilisema hakuumia sana, lakini vipimo vimeonyesha tofauti na ilivyoripotiwa.

"Tunaimani ataweza kurudi kabla ya msimu huu, lakini hatuna uhakika sana katika hilo."

Martial aliumia goti akiwa na timu ya Taifa ya Ufaransa katika michezo ya kufuzu Fainali za Kombe la Dunia 2022 zitakazofanyika nchini Qatar.

# *Mourinho: Spurs imekosa utulivu*

**LONDON,** England

JOSE Mourinho amekiri kwamba, Tottenham Hortspur inakabiliwa na makosa mengi na kwamba, timu yake hiyo "hukosa utulivu" mara kwa mara, baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 na Newcastle United kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Harry Kane alifunga mabao mawili kipindi cha kwanza baada ya goli la Joelinton, lakini Spurs haikuweza kumaliza mechi hiyo kwa ushindi pale St. James 'Park, kwani Joe Willock aliisawazishia Newcastle dakika ya 85.

"Nimefadhaika," alisema Mourinho akiiambia BBC Radio 5Live.

"Tulihitaji kushinda mechi na tulikuja kushinda. Hatukuwa mbali, lakini wakati huo huo, hatukuwa na utulivu na makosa mengi ya kujihami.

"Kila wakati tuliipa Newcastle nafasi ya kuwa kwenye mchezo.

"Tulikuwa na nafasi kubwa ya mchezo kuufanya uwe 3-1 na kumaliza shughuli wakati Kane alipogongesha mpira kwenye goli na kisha tukaruhusu bao dakika iliyofuata.

"Tunafanya kazi vizuri, tunafanya kazi kwa bidii. Lakini kuna makosa ambayo labda haifai hata kuyaita makosa kwa sababu yanahusiana na sifa ambazo wachezaji wanazo. Unaweza kuchanganua kwa urahisi."




# Casemiro aitabiria Madrid mataji yote




**MADRID,** Hispania

KIUNGO wa Real Madrid, Casemiro, amebainisha kwamba, klabu hiyo inaweza kushinda mataji yote mawili ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya, msimu huu.

Mbio za kuwania taji la LaLiga zilirejea Jumamosi ambapo Real Madrid waliwafunga Eibar mabao 2-0, hivyo 'Los Blacos' hao sasa wapo nafasi ya pili kwenye msimamo kwa tofauti ya alama tatu nyuma ya viongozi Atletico Madrid na sasa wamebakiza mechi tisa ligi imalizike.

Real Madrid leo Jumanne watarejea pia katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool ikiwa ni hatua ya robo fainali ya mchezo wa kwanza.

"Kila mtu anajua nini ambacho tunakiweza na nini tunaweza tukakifanya," alisema Casemiro akiiambia TVE.

"Tutapambana hadi mwisho, tunajua hilo ni gumu sana, lakini tutapambania mataji yote.

"Kwa Real Madrid michezo yote ni muhimu tumekuwa tukicheza mechi kubwa."

Mchezaji huyo raia wa Brazil alikuwa kikosi cha Madrid waliposhinda mataji ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara tatu mfululizo kutoka mwaka 2016 mpaka 2018.

## HABARI MICHEZO

# Pulisic aipa pigo Chelsea

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amethibitisha kuwa Christian Pulisic alipata majeraha ya misuli ya nyama za paja wakati Chelsea ilipofungwa mabao 5-2 nyumbani na West Brom, Jumamosi.

Nyota huyo wa Marekani amepata majeraha hayo na atapimwa na timu ya matabibu ya klabu kabla ya wiki za mwisho za msimu.

"Christian alikimbia wakati aliporudi kwa ajili kipindi cha pili na akasema kwamba alihisi msuli wake unashida na asingeweza kudumu hadi mwisho wa mchezo," alisema Tuchel akiwaambia waandishi wa habari.

"Kwa hiyo ilibidi tuchukue uamuzi wa kumbadilisha mara moja," aliongeza.

Changamoto hii ya majeraha inakuwa jeraha lake la nne la misuli msimu huu na la nane kwa jumla tangu ajiunge na Chelsea mnamo mwaka 2019.

Tuchel ana matumaini ya kupungua kwa majeruhi kuelekea mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa dhidi ya Porto, Jumatano.






# DE GEA RASMI KUONDOKA UNITED

**MANCHESTER,** England

GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, anatarajiwa kuondoka mwishoni mwa msimu huu sambamba na malipo makubwa ya kumaliza mkataba wake.

Na sasa Dean Henderson atakuwa rasmi golikipa chaguo la kwanza kwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Kwa mujibu wa gazeti la The Mirror, United iko tayari kuachana na De Gea mwenye umri wa miaka 30, ambaye analipwa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Akiwa amebakiwa na miaka miwili kukamilisha mkataba wake, hatua yoyote ya Mashetani Wekundu ya kusitisha mkataba wa De Gea inaweza kuhusisha malipo makubwa ili kupunguza muda wake pale Old Trafford.

Mara baada ya kuwa mchezaji bora kwenye kikosi cha Man United, na mchezaji anayelipwa mshahara mkubwa zaidi klabuni hapo, kiwango cha De Gea kimeshuka sana katika misimu michache iliyopita.

Henderson ametoka kucheza kwa mafanikio kwa mkopo kule Sheffield United msimu uliopita, na amesaini mkataba wa miaka sita ambao unamfanya alipwe mshahara wa pauni 120,000 kwa wiki.

# *Lacazette sasa kujua moja Arsenal mwisho wa msimu*

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema hatima ya mshambuliaji wake, Alexandre Lacazette itaamriwa mara baada ya msimu huu kumalizika.

Mkataba wa sasa wa Lacazette na Arsenal utamalizika Juni mwakani na ilitegemewa 'Washikabunduki' hao wangekuwa wanafanya naye mazungumzo ili aongeze mkataba kuendelea kuichezea kutokana na kiwango bora anachokionyesha

Hata hivyo, Arteta amefichua kuwa mazungumzo ya Arsenal na Lacazette yamesimama na yataendelea baada ya msimu kumalizika na akili yao kwa sasa ni kufanya vizuri katika mechi zilizobakia.

"Suala la Laca tutalishughulikia wakati wa majira ya joto. Tutazungumza naye na kupendekeza nini kinahitajika kwa siku za usoni," alisema Arteta akinukuliwa na Sky Sport.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR AZIWEKA KATIKA MIZANI PSG, BARCELONA

### ●●● Atacheza tena na Messi, lakini si hapo Paris bali pale Camp Nou, na tayari...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa Paris Saint-Germain, Neymar Jr, ameiweka njiapanda klabu hiyo baada ya kusimamisha mazungumzo yake ya kuongeza mkataba klabuni hapo, kwani anaanza kufikiria kwamba, Lionel Messi atabaki Barcelona.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, amekuwa wazi katika nia yake ya kuungana tena na Messi, na ripoti nyingi mwanzoni mwa mwaka zilihusisha raia huyo wa Argentina kwenda PSG.

Lakini gazeti la Ara la Catalunya limeripoti kwamba, Neymar si tu anaamini kuwa Messi ataongeza mkataba juu ya makubaliano mapya pale Camp Nou, lakini pia Mbrazil huyo amewaarifu Barcelona kuwa yupo tayari kurudi klabuni hapo.

**Hii ni sawa na taarifa zilizotolewa na skauti wa zamani wa Barcelona, Andre Cury.**

"Neymar atacheza tena na Messi, si kwenye klabu ya PSG bali Barcelona," Cury alinukuliwa El Litoral mwezi uliopita.

Hata hivyo, kurudi kwa Neymar Barcelona kunaweza kuwa kugumu kutokana na hali ya kifedha ya klabu hiyo kwa sasa, ingawa atakuwa tayari kujitolea ili kusukuma hatua hiyo.

Wakurugenzi wa 'Blaugrana' hao pia wanamfutilia mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Haaland na straika wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

## ZISIKUPITE

### SOLSKJAER AMKATAA AGUERO

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema mshambuliaji wa Argentina, Sergio Aguero mwenye umri wa miaka 32, hatajiunga nao baada ya mkataba wake na wapinzani wao Manchester City kumalizika mwishoni mwa msimu. ***(Goal)***

### MILENKOVIC ATAKIWA EPL

LIVERPOOL na Manchester United zinawania kumsajili mlinzi wa Fiorentina, Nikola Milenkovic mwenye umri wa miaka 23. ***(Corrierre Fiorentina, via Team Talk)***

### LAPORTA KUAMUA KWA HAALAND

KOCHA wa Barcelona, Ronald Koeman, amesema suala la Erling Haaland mwenye umri wa miaka 20, kutua klabuni hapo kutategemea na uamuzi wa Rais Joan Laporta. ***(AS)***

### MESSI SASA ASUBIRIA OFA

LIONEL Messi anasubiri ofa atakayopewa na Rais Joan Laporta ili kuamua kama atabaki Barcelona au kwenda PSG ama Manchester City. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### RODGERS AMUWANIA MCGREGOR

KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers, ana matumaini ya kumsajili kiungo wa Scotland, Callum McGregor mwenye umri wa miaka 27, kutoka Celtic. ***(Sun)***

### MOYES KUMUUZA RICE

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema atasikiliza ofa kwa Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, na kiungo Tomas Soucek mwenye, 26. ***(Mirror)***

### DEMBELE AGEUKA LULU

KLABU za Manchester United na Juventus zimeonyesha nia ya kutaka kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele, mwenye umri wa miaka 23, lakini Liverpool na PSG pia zinamtaka. ***(Mundo Deportivo)***

### DI MARIA AMTAKA MESSI

ANGEL di Maria amesema atapenda kucheza sambamba na raia mwenzake wa Argentina, Lionel Messi, 33, pale PSG kama mchezaji huyo ataamua kuondoka Barcelona. ***(beIN Sports, via Goal)***

### VAZGUEZ AGOMBEWA ULAYA

WINGA wa Hispania, Lucas Vazquez, 29, ambaye mkataba wake na Real Madrid unamalizika mwishoni mwa msimu huu, anawaniwa na Manchester United, Chelsea, AC Milan pamoja na Bayern Munich. ***(ABC - in Spanish)***

### MORATA KUONDOKA JUVE

JUVENTUS hawana uwezekano wa kulipa pauni milioni 8.5 zaidi kwa Atletico Madrid kwa ajili ya kuongeza mkataba wa mshambuliaji wa Hispania, Alvaro Morata kwa mwaka mmoja mwingine kwa sababu ya changamoto za kifedha. ***(AS)***

## HABARI MICHEZO

## Gwambina yataka 6 kutoka Simba, Yanga

**Na Saada Akida**

WAKATI Ligi Kuu Bara ikitarajiwa kurejea keshokutwa Alhamisi, ikiwa ni baada ya kumalizika kipindi cha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Klabu ya Gwambina ya Misungwi, Mwanza, imesema malengo yao ni kuvuna pointi tisa katika michezo minne watakayocheza mwezi huu ikiwamo dhidi ya Simba na Yanga.

Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Mohammed Badru, amesema malengo makubwa kwao ni kuhakikisha wanapata pointi tisa au zaidi katika michezo minne ya mwezi huu wakianza na Coastal Union, watakapoikaribisha Aprili 10, kabla ya kufunga safari hadi Dar es Salaam dhidi ya KMC FC , Aprili 16.

Alisema baada ya hapo watavaana na Yanga Aprili 20 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa na siku nne baadaye watakuwa nyumbani kuikaribisha Simba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Badru alisema ameandaa kikosi chake kwa ajili ya kwenda kutafufa matokeo mazuri katika michezo hiyo lengo la kwanza likiwa ni kuvuna alama tisa.

Alisema ni vizuri kupata pointi zote 12 katika michezo hiyo minne, ila mipango yake ya awali ni kusaka pointi tisa kwa kutafuta matokeo nyumbani na ugenini.

"Nina imani ya kupata pointi hizo au zaidi kwa sababu ya morali na uwezo wa wachezaji wangu unanipa matumaini ya kufanya vizuri, sasa hivi sitacheza kwa kuzuia kama ilivyokuwa katika michezo ya awali, bali nitacheza kwa nidhamu ya hali ya juu kuzuia na kufanya mashambulizi kwa wapinzani wetu," alisema Badru.

Gwambina FC iko nafasi ya 11 baada ya michezo 22 wakiwa na pointi 27 sawa na Coastal Union iliyopo nafasi 12 lakini yenyewe ikiwa imeshuka dimbani mara 23 kwenye ligi hiyo inayojumuisha timu 18 msimu huu.

# MWAMEJA AIONA SIMBA YA MWAKA 1993 MWAKA HUU

**Na Adam Fungamwango**

KIPA wa zamani wa Simba, Mohamed Mwameja, amekifananisha kikosi cha mwaka huu cha timu hiyo na cha mwaka 1993 ambacho kilifika fainali za Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na yeye akiwamo.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwameja ambaye enzi zake dimbani akijulikana kama 'Tanzania One', pia amemsifia kipa Aishi Manula na kusema kuwa kwa sasa anastahili kuwa 'Tanzania One' kutokana na uwezo mkubwa alionao.**

Mwameja ambaye alikuwamo kwenye kikosi cha Simba kilichofika fainali ya CAF mwaka 1993 na kufungwa mechi ya pili ya fainali jijini Dar es Salaam mabao 2-0, baada ya kutoka suluhu nchini Ivory Coast dhidi ya Stella Abidjan na kulikosa kombe hilo, alisema kuwa kasoro ndogo iliyopo ni kwamba wakati huo walikuwa ni wachezaji wazawa, tofauti na sasa ambapo wengi wao ni wa kigeni.

"Kusema kweli niipongeze Simba kwa kupeperusha vema bendera ya Tanzania, ni furaha kwa Watanzania wote na niseme tu kuwa hiki ni moja kati ya vikosi bora kabisa kuwahi kutokea. Hiki naweza kukifananisha na kile cha kwetu cha 1993. Kasoro tu labda ni kwamba wa sasa wengi ni wa kigeni, lakini sisi wote tulikuwa ni Watanzania," alisema.

Aliwataka wachezaji wa Simba wasiridhike na mafanikio ambayo yamepatikana, badala yake wapambane ili waweze kufika fainali.

"Kwa kikosi cha Simba cha sasa, kina uwezo kabisa wa kufika fainali, wachezaji wapambane tu," alisema Mwameja.

Kuhusu Manula, alisema kuwa hivi sasa amebadilika si yule ya miaka miwili iliyopita.

"Inawezekana ni kwa sababu ya kocha wa makipa aliyekuja. Naona amembadilisha sana. Hivi ndivyo inavyotakiwa. Kipa na nafasi ya ulinzi kama mkiwa vizuri, timu ina uwezo mkubwa wa kushinda mechi," alisema.

Jumamosi iliyopita, Simba iliichapa AS Vita mabao 4-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika huku ikiongoza kundi lake la A na ikiwa imebakiza mechi moja ugenini dhidi ya Al Ahly ya Misri kabla ya kukamilisha hatua ya makundi.

**UMEFUNIKA...**



Ofisa Uhusiano na Masoko wa Emirates Aluminium, Issa Maeda (Kulia), akimkabidhi beki wa Simba, Joash Onyango, tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwezi wa klabu hiyo baada ya kutangazwa mshindi wa Machi akiwapiku kipa Aishi Manula na winga Luis Miquissone. **PICHA: SIMBA**

# *Morocco atoa sababu vichapo Namungo CAF*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco, amesema kutokuwapo kwa wachezaji wenye uzoefu wa kucheza michuano ya kimataifa ni sababu kubwa kwa timu yake hiyo kutopata matokeo mazuri katika michezo mitatu ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika waliyocheza hadi sasa.

Namungo juzi ilikubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Nkana FC ya Zambia katika mechi ya Kundi D ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, huo ukiwa ni mchezo wa pili mfululizo kupoteza nyumbani bada ya uliopita kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Pyramids ya Misri dimbani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema si malengo yao kupoteza mechi tatu, mbili nyumbani na moja ugenini, ila balaa hilo limewakumba kutokana na ugeni wa timu hiyo katika michuano hiyo.

Alisema kukosekana kwa aina ya wachezaji wazoefu wa michuano ya kimataifa kwenye timu yake, kumechangia kutopata matokeo mazuri mbele ya timu ambazo wanakutana nazo,

"Ukiangalia timu ambazo tuko nazo kundi moja, zina uzoefu mkubwa wa hii michuano pamoja na aina ya wachezaji wao, tofauti na timu yangu ambayo bado ni changa wakati huu tukiijenga timu.

Alisema ana imani baada ya michuano hii, wachezaji wake watakuwa wamepata uzoefu kidogo ambao utawasaidia kujipanga kwa mechi zijazo.

Kikosi cha Numungo kimebakiza michezo mitatu katika michuano hiyo miwili ugenini; dhidi ya ya Nkana FC, Aprili 11 na watarejea nyumbani kuikaribisha Raja Casablanca ya Morocco Aprili 21, ambayo iliwafunga ba 1-0 katika mechi ya awali, kabla ya Aprili 28, mwaka huu kwenda nchini Misri kuhitimisha mechi za makundi kwa kuivaa Pyramids.

Michezo
Nipashe
Jumanne Aprili 6, 2021



Neymar aziweka katika mizani PSG, Barca UKURASA 22

HUPATI KITU!...



Kipa wa Brighton & Hove Albion, Robert Sanchez, akiucheza mkwaju wa kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandes, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na wenyeji hao kuibuka na ushindi wa mabao 2-1. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yatisha vigogo CAF

## ●●● Kocha wa Wydad Casablanca anayochezea Msuva, asema hatamani kukutana nayo kwa sasa, huku...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI miamba yenye dhamana ya kuipeperusha bendera ya Tanzania na Afrika Mashariki na Kati, kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, Simba, ikiwa tayari imetinga robo fainali ya michuano hiyo, muziki wake umeanza kuvitisha vigogo vya soka katika soka la Afrika, imefahamika.

**Simba ambayo ni timu pekee iliyobaki katika Ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati kwenye michuano hiyo, imeongoza msimamo wa Kundi A ambalo lilifahamika kama kundi la kifo, kutokana na kujumuisha timu ngumu na zenye uzoefu mkubwa katika michuano hiyo, ikiwamo bingwa mtetezi, Al Ahly ya Misri, AS Vita ya DR Congo na Al-Merrikh ya Sudan.**

Na timu zote hizo zimechezea kichapo katika Uwanja wa Benjamin Mkapa huku AS Vita yenyewe ikipigwa nyumbani na ugenini na Al-Merrikh ikiambulia sare tasa nyumbani, huku Al Ahly ikiwa na kibarua kigumu cha kuhakikisha inaepuka kupingwa nyumbani na ugenini itakapoikaribisha Simba Ijumaa wiki hii kwenye mechi ya kuhitimisha hatua ya makundi.

Wakati droo ya hatua ya robo fainali ikitarajiwa kupangwa Aprili 30, mwaka huu, Wydad Casablanca, moja ya timu kongwe, ngumu na yenye uzoefu mkubwa katika michuano hiyo na mabingwa wa mwaka 2017, wamepaza sauti yao wakiomba na kupiga hesabu kali kuepuka kukutana na Simba katika hatua inayofuata.

Mabingwa hao wa Morocco, Wydad Casablaca, ambao anaichezea Mtanzania Simon Msuva, wapo kileleni mwa msimamo wa Kundi D wakiwa na alama 10, huku Horoya AC ya Guinea, Kaizer Chief ya Afrika Kusini kila moja ikiwa na pointi nane wakati Petro de Luanda ya Angola ikiburuza mkia na pointi yake moja.

Matokeo ya mechi zao za Jumamosi ndiyo yataamua timu itakayoongoza kundi na itakayoshika nafasi ya pili wakati Wydad ambayo imeshafuzu robo fainali, itaikaribisha Petro de Luanda ikihitaji ushindi ili kuongoza Kundi A, huku Horoya AC ikiwa mwenyeji wa Kaizer Chiefs, mchezo ambao utaamua timu itakayotinga hatua inayofuata.

Kwa mujibu wa kanuni za michuano hiyo, timu zitakazoongoza makundi yao, katika droo itakayochezeshwa zitakutana na washindi wa pili kutoka katika kila kundi, lakini pia zilizopo kundi moja hazitakutana.

Hata hivyo, kama Wydad itapoteza mchezo huo na ama Horoya au Kaizer Chiefs mojawapo ikashinda, moja kwa moja mabingwa hao wa Morocco watashika nafasi ya pili na kuwa katika hatihati ya kukutana na Simba wakati droo ya robo fainali itakapochezeshwa Aprili 30.

Lakini baada ya mechi ya Jumamosi ambayo Wydad ilikubali kipigo cha bao 1-0 ugenini dhidi ya Kaizer Chiefs, Kocha Mkuu wa miamba hiyo ya Morocco, Faouzi Benzarti, akizungumza na vyombo vya habari, aliitaja Simba kuwa ni moja ya timu ngumu na tishio barani Afrika, hivyo hatamani kukutana nayo mapema. Benzarti alisema si Simba tu bali timu yoyote iliyopo katika michuano hiyo, kila moja ina lengo la kufika fainali ama kutwaa ubingwa, lakini hawataki kabisa kukutana na mabingwa hao wa Tanzania katika hatua ya robo fainali ama nusu fainali, kwa kuwa lolote linaweza kutokea.

Alisema kwa sasa Simba ina timu nzuri na inacheza kwa mbinu sana na kwamba ili kuishinda lazima ujipange vilivyo.

## Yanga SC kuikwepa mbeleko Simba CAF

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa itakwenda kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao kwa nguvu zao wenyewe na wala si kwa kubebwa na timu yoyote ile.

Kitendo cha Simba kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kimeiongezea Tanzania pointi na sasa ipo katika nafasi ya kuingiza timu nne kwenye michuano ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF); timu mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho.

Bingwa wa Ligi Kuu Bara, hukata tiketi ya moja kwa moja kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika huku mshindi wa Kombe la FA, akikata tiketi ya Kombe la Shirikisho na timu inayoshika nafasi ya pili na tatu ndizo hupewa dhamana ya michuano ya kimataifa endapo Tanzania ikiwa na tiketi ya kuingiza timu nne.

Lakini Ofisa Habari wa Yanga, Hasan Bumbuli, amesema kuwa nia yao msimu huu ni kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa tiketi yao wenyewe na si ya kukatiwa na timu nyingine.

Bumbuli alisema hayo alipoulizwa juu ya ushindi wa Simba wa mabao 4-1 dhidi ya AS Vita iliopata Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao umeiweka Tanzania kwenye mazingira mazuri ya kuongeza timu msimu ujao kwenye michuano ya kimataifa.

"Mimi sijasikia matokeo yoyote ya Simba. Ila kama wameshinda basi sawa, lakini kusema eti watatubeba kwenye mechi za kimataifa, labda wawabebe wengine siyo sisi. Yanga tutakwenda kwa nguvu zetu wenyewe kwenye michuano ya kimataifa kwa sababu kwa sasa tunaongoza ligi na tunausaka ubingwa, nina imani tutaupata na hatutohitaji kutafutiwa nafasi na mtu," alisema Bumbuli wakati huu timu yao ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu na pointi 50 ikifuatiwa na Simba yenye alama 46, lakini ikiwa nyuma kwa michezo mitatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >